# Nipashe

Jumamosi Machi 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580875

www.ippmedia.com

MWANGA WA J

www.twitter.com/nipashetz

stagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US









**Adaiwa** kumuua mke wake kisha 'kujipiga kitanzi'

UKURASA 5



**MKHITARYAN ATANGAZA KUTUNDIKA DARUGA**

UKURASA 22

# IMEKWISHA

• **DPP** ahitimisha siku 221 za Mbowe jela, mwanawe, wakili watoa ya moyoni, viongozi wa dini, wanasiasa, wanasheria watia neno... *Endelea ukurasa 2 & 3*



Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu.




**"Tanzania iwe mahali ambapo haki inapigana busu na amani.**



**"Kufutwa kwa kesi dhidi ya Mbowe ni fursa kwa Tanzania.**



**"Haya ni mafanikio makubwa, kwa kweli tumefarijika.**



**"Sheria ibadilike, mtu asikamatwe ndipo muanze uchunguzi.**



**"Mahakama imetekeleza sheria, msiweke siasa kwenye mambo ya sheria.**





Wafuasi na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakishangilia nje ya makao makuu ya chama hicho, Mtaa wa Ufipa, Kinondoni, Dar es Salaam jana, baada ya kupata taarifa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Freeman Mbowe na wenzake, wameachiwa huru katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. **Kulia,** Mbowe na wenzake wakiwa nje ya gereza la Ukonga baada ya kuachiwa **PICHA: JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** **MAYELE : NI MSIMU WA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Imekwisha, siku 221 za Mbowe gerezani

**Na Kulwa Mzee**

IMEKWISHA! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake watatu waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka matano ya ugaidi kuachiwa huru bila masharti.

Vifijo na nderemo jana asubuhi vilitawala ndani na nje ya Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mkoani Dar es Salaam baada ya amri ya kuwaachia huru washtakiwa kutolewa huku wenyewe wakiwa hawako mahakamani kwa madai kwamba Mbowe alipata tatizo la kiafya.

Jopo la Mawakili wa utetezi likiongozwa na Peter Kibatala liliibuka kushangilia huku likiimba "sitasimama maovu yakitendeka, ufisadi, ubinafsi, ukabila, wauza sura hawataki kuuza sera, udugu ni kufaana, sitasimama maovu yakitendeka".

Mahakama hiyo mbele ya Jaji Joackim Tiganga iliwaachia huru washtakiwa hao baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kuwasilisha hati (Nolle Prosequi) akionyesha hana nia ya kuendelea na shauri hilo, hivyo kuhitimisha siku 221 za Mbowe kukaa mahabusu gerezani tangu Julai 26 mwaka jana alipounganishwa na washtakiwa wenzake.

Shauri hilo lilikuja kwa ajili ya washtakiwa kuanza kujitetea lakini washtakiwa hawakuwako mahakamani na ilitolewa taarifa na ofisa wa magereza kuwa Mbowe amepata tatizo la kiafya, hivyo asingeweza kuwako mahakamani lakini upande wa mashtaka uliomba kutoa taarifa yao.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, aliomba kuwasilisha maombi yao na mahakama iliruhusu.

"Mheshimiwa Jaji, Mkurugenzi wa Mashtaka nchini kwa niaba ya Jamhuri anaomba kuwasilisha taarifa ya kutokuwa na nia ya kuendelea na shauri hili.

"Taarifa hii tunaitoa chini ya kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, tunaomba kuondoa mashtaka yote dhidi ya washtakiwa wote, sababu zote zipo katika hati ambayo tumewasilisha," alidai Kidando.

Kifungu hicho kinasema: "Katika sheria yoyote ya jinai na katika hatua yoyote ile kabla ya hukumu au uamuzi, kama itakavyokuwa, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuweka 'nolle prosequi', aidha kwa kueleza mahakamani au kuiambia mahakama husika kwa maandishi kwa niaba ya Jamhuri kuwa mwenendo hautaendelea.

"Na baada ya hapo mtuhumiwa ataachiwa mara moja kuhusiana na shtaka ambalo nolle prosequi imewekwa na kama amepelekwa gerezani atatakiwa kuachiwa, au kama yuko chini ya dhamana, wadhamini wake watakoma kuwa wadhamini." Jeremiah Mtobesya ambaye ni Wakili wa Mshtakiwa wa Kwanza, Halfani Bwire, alipotakiwa kujibu, alidai wamesikia hoja iliyowasilishwa na DPP na kwa bahati mbaya hawawezi kusema lolote.

Alidai wanaiachia mahakama kwa sababu kifungu hicho kinatoa maelezo yote, wanaiachia mahakama dhidi ya amri zake za mwisho.

Wakili wa Mshtakiwa wa Pili, John Mallya, alidai notisi iliyotolewa inawafunga mikono, hawawezi kusema lolote, walitaka sana warudishiwe gharama zao na mengine lakini wanasubiri uamuzi wa mahakama.

Wakili wa Mshtakiwa wa Tatu, Fredrick Kihwelo, alidai wanaiachia mahakama kwa kuwa sheria inajieleza wazi na Wakili Peter Kibatala pia alidai wanaiachia mahakama.

Jaji Tiganga baada ya kusikiliza pande zote mbili, alisema mahakama imesikia hoja iliyotolewa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Kidando, kuwa DPP hana nia ya kuendelea na shauri na upande wa pili ukaridhia.

"Shauri hili lina washtakiwa Halfani Bwire, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Freeman Mbowe, linaondoshwa mahakamani na washtakiwa wanaachiwa huru bila masharti.

"Kwa sababu kuna vielelezo vililetwa mahakamani, ninaandaa amri ya kuviachia, ninaelekeza Mkuu wa Magereza kuwaachia mara moja leo (jana) na si vinginevyo," Jaji Tiganga alitoa amri.

Kabla ya maombi hayo, Wakili Kibatala na jopo lake walidai mahakamani kwamba walijipanga vizuri kuanza utetezi na walikuwa wanatarajia kuita jumla ya mashahidi 27 na vielelezo 35 huku upande wa Jamhuri ukifunga ushahidi ukiwa na mashahidi 13.

Washtakiwa walikuwa wanatuhumiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei na Agosti 5, 2020 maeneo ya Moshi, Arusha, Mbeya, Morogoro, Dar es Salaam na Mwanza.

Kesi yao ilianza kusikilizwa Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Agosti 31, 2021 mbele ya Jaji Elinaza Luvanda.

Septemba 6, 2021, Jaji Luvanda alijitoa kuendelea kusikiliza kesi hiyo baada ya Mbowe kumwomba ajitoe ili kulinda heshima yake kwa kuwa hakuwa na imani naye.

Shauri hilo lilihamia kwa Jaji Mustapha Siani, Septemba hadi Oktoba lakini jaji huyo aliteuliwa kuwa Jaji Kiongozi na akaomba shauri lipangiwe jaji mwingine kwa kuwa kutokana na majukumu yake asingepata muda wa kuisikiliza.

Shauri lilihamia kwa Jaji Tiganga hadi jana lilipoondolewa na kuwaachia huru washtakiwa.

Maombi ya DPP na uamuzi wa Mahakama ulionekana kuwafurahisha wafuasi wa ChHADEMA ambao walikuwa wamehudhuria mahakamani kufuatilia kesi hiyo.

"Tulitegemea haya matokeo ya leo kutokana na maombi ya viongozi wa dini na wanasiasa pamoja na wananchi wengine kuomba Mbowe aachiwe," alidai Mwita Paul.

## Mtoto wa Mbowe, Kibatala watoa ya moyoni

**Na Romana Mallya**

JAMES Mbowe, mtoto wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Freeman Mbowe, amesema amekuwa akihudhuria kesi ya baba yake tangu ilipoanza hadi jana Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) aliposema hana nia ya kuendelea na shauri hilo.

Wakati James akisema hayo, kiongozi wa jopo la mawakili wa mwanasiasa huyo, Peter Kibatala, alitoa machozi baada ya hitimisho la kesi hiyo huku akibainisha kuwa haikuwa kazi rahisi katika kumtetea Mbowe na wenzake.

"Kutoka mwanzo, mzee alipokamatwa Mwanza, namna ya ukamataji, alivyovamiwa hotelini mlango ukavunjwa akasafirishwa Dar es Salaam, akapelekwa Kisutu kisha gerezani na alipoanza kuhudhuria kesi hii, sijakosa hata siku moja mahakamani.

"Wana-CHADEMA wamefurahi sana na mimi nikiwa mmoja wa waliofurahi. Lakini nimefurahi wakati huo huo nikiwa na maumivu kwa sababu mzee amekaa ndani kipindi chote hakuwa anastahili kuwa pale. Ni kiongozi mkubwa wa chama na baba wa familia," alisema.

Alisema kesi ya baba yake ilikuwa kama wote wamefungwa kwa sababu ya kutumia muda mwingi kushinda mahakamani.

"Unashinda mahakamani kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa halafu Jumamosi na Jumapili uende gerezani kumtembelea. Kwa niaba ya familia tunamshukuru Mungu.

"Siku ngumu sana ilikuwa ni ile upande wa Jamhuri ulipofunga ushahidi wao. Wengi walitegemea mzee na wenzake hawatakuwa na kesi ya kujibu. Ni siku ambayo sintosahau," alisema.

Akizungumza nje ya mahakama baada ya Jaji kutangaza kuwaachia wateja wao bila masharti, Wakili Kibatala alisema wametoa jasho na damu, mioyo na roho.

"Dickson Matata anakuja kwenye kesi huku mke wake amefanyiwa upasuaji anampeleka hospitali asubuhi, anakuja mahakamani kwa kipindi chote cha miezi mitano.

"Kipekee kabisa tunamshukuru Askofu (Erasmus) Mwamakula. Hukukaa ofisini, hukukaa kanisani ulikaa na sisi siku zote. Wateja ni bora pamoja na magumu lakini wamekuwa watulivu. Kesi hii haikuwa ndogo madhara yake yangeweza kuwa makubwa hasa vijana walikuwa na vitu vingi vya kupoteza.

"Wamepitia vitu ambavyo vimewa 'traumatize' (vimewapa msukosuko wa akili). Ushahidi wao mliusikia namna walivyokamatwa walihadithia ulimwengu waliyopitia lakini walikabidhi hatima zao mikononi mwetu na hatujawaangusha.

"Tumeacha kila kitu chetu, kila ujuzi wetu kila uimara wetu. Tunaamini hatua hii imefikiwa kwa kazi kubwa tuliyoifanya," alisema.

Akieleza alichopitia katika kesi hiyo ambacho hatosahau, Wakili Kibatala alisema inamkumbusha kuwa hiyo ilikuwa kesi yake ya tatu ya ugaidi.

"Kesi ya kwanza niliendesha ya (Wilfred) Lwakatare baadaye akaachiwa huru. Kesi ya ugaidi Tabora ilikuwa ya pili nao wakaachiwa huru. Hii ilikuwa na 'impact' kidogo. Tulijitahidi jopo lote kutumia ujuzi wetu wote. Hata kama kulikuwa na mabonde tulifahamu safari yetu itakwenda kuishia wapi," alisema.

### ALIA MAHAKAMANI

Akizungumzia kuhusu kitendo chake cha kulia baada ya kufutwa kwa kesi hiyo jana, Wakili Kibatala alisema ilikuwa safari ndefu na haikuwa kazi rahisi kuendesha kesi ya Mbowe inayotazamwa kitaifa na kimataifa.

"Ilikuwa traumatic experience (uzoefu wa misukosuko) tumepitia mambo mengi kwa hiyo kuna muda unashindwa kuzuia hisia," alisema.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya mafanikio ya Wizara hiyo, katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuanzia Machi 2021 hadi Februari 2022. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Viongozi wa dini, balozi, wanasiasa, watoa kauli

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya viongozi wa dini, wanasiasa na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, wametoa maoni yao kuhusu kuachiwa huru kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya ugaidi.

Muda mfupi baada ya Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kuwaachia huru washtakiwa hao jana, Nipashe ilizungumza na viongozi hao, kila mmoja akiwa na mtazamo wake.

PIUS MSEKWA

Aliyekuwa Spika wa Bunge, Pius Msekwa, alisema kuachiwa huru kwa Mbowe ni sehemu ya mahakama kufanya kazi yake kwa mujibu wa sheria.

Msekwa alisema mahakama imefanya kazi yake na hakuna sababu ya kuingiza siasa katika sheria.

"Hakuna kupinga wala kuunga mkono, ni kutambua mahakama imefanya kazi yake. Kifungu alichokitumia DPP (Mkurugenzi wa Mshtaka) kufuta kesi hata mimi nakijua.

"Sheria aliyoitumia siyo kwa kesi hii tu, zipo kesi nyingine ambazo washtakiwa waliachiwa huru kwa kifungu hicho alichokitumia katika kesi ya kina Mbowe," alisema.

Msekwa aliongeza: "Ni mahakama inatekeleza sheria, msiweke siasa kwenye mambo ya sheria. Itambulike mahakama inatekeleza sheria."

**ZITTO KABWE**

Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Zitto Kabwe, alisema amefarijika baada ya kuona Mbowe ameachiwa huru dhidi ya kesi ya ugaidi iliyokuwa ikimkabili.

"Kama mtakumbuka, maoni yangu niliyoyatoa wakati wa mkutano wa Rais (Samia Suluhu Hassan) kule Dodoma, nilizungumza kwa niaba ya TCD niliomba viongozi wote tuwapo na ni matarajio yangu mkutano ambao Rais anakuja kuufanya Dodoma kwenye ukumbi ule ambao tuliomba viongozi wote tuwapo, tutakuwapo.

"Haya ni mafanikio makubwa, kwa kweli tumefarijika, tunaamini tutakwenda pamoja turejeshe demokrasia yetu na tujenge upya misingi ya demokrasia," alisema.

**BALOZI MAREKANI**

Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, baada ya kutolewa kwa uamuzi wa kuachiwa huru kwa kina Mbowe, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Kufutwa kwa kesi dhidi ya Freeman Mbowe leo (jana) ni fursa kwa Tanzania kubadili ukurasa na mwelekeo wake wa baadaye.

"Tuendelee kushirikiana kutumia fursa nyingi zilizopo na kujenga amani, ustawi na uhuru kwa wote."

**ASKOFU BAGONZA**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, alishauri kumulikwa kwa sheria za nchi ili sheria iliyowanyima dhamana kina Mbowe irekebishwe.

"Niwakumbushe mwezi Februari 1990, Nelson Mandela akatolewa jela akaja Tanzania kushukuru, tukajipanga na mabango na kushangilia "Mandela is free" (Mandela yuko huru).

"Akasimama Kambarage (Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere) akasema 'Mandela is not free, he is out from prison' (Mandela hayuko huru, yuko nje ya gereza). Kwa nini? Kwa sababu sheria iliyomweka gerezani miaka 27 bado ipo, haijafutwa.

"Mbowe ametoka gerezani alimokaa miezi minane. Watu wanashangilia kuwa Mbowe yuko huru. Mimi ninasema hayuko huru, bali yuko nje ya gereza kwa sababu sheria iliyomshtaki na kumnyima dhamana bado haijafutwa.

"Punguzeni mashangilio, boresheni fikra na mikakati ya kuifanya Tanzania kuwa mahali ambapo haki inapigana busu na amani," alisema.

Askofu Bagonza pia alitumia nafasi hiyo kumpa pole na wakati huo huo kumpongeza Mbowe huku akimtakia heri Rais Samia Suluhu Hassan wakati akikaribia kutimiza mwaka mmoja wa uongozi wake Ikulu.

Askofu Bagonza alikuwa miongoni mwa viongozi wa dini walioshiriki mkutano na Rais Samia siku mbili zilizopita Ikulu jijini Dar es Salaam, wakiomba mamlaka husika zitumie busara kuimaliza kesi hiyo dhidi ya Mbowe na wenzake.

■**Imeandikwa na Romana Mallya, Mary Geofrey na Beatrice Shayo**

# Wanasheria, wanaharakati wafunguka

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wanasheria na wanaharakati, ikiwamo watetezi wa haki za binadamu, jana walitoa maoni yao kuhusu kufutwa kwa kesi ya ugaidi iliyokuwa ikimkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wenzake watatu.

Miongoni mwa wanasheria waliotoa maoni ni Rais Mstaafu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, ambaye alisema hatua iliyofikiwa ni nzuri huku akibainisha kwamba hata mashtaka yenyewe hayakuwa na ushahidi wa kutosha.

Alisema kutokana na hali hiyo, Mkurugenzi wa Mashtaka aliona amwachie kwa sababu watu wa kada mbalimbali wamekuwa wakihimiza kuachiwa kwake kutokana na kuwa kesi haina tija kwa maslahi ya taifa, amani na usalama wa nchi.

"Msingi wake haukuwapo na ushahidi wake uliotolewa ulikuwa dhaifu sana. Lakini watu mbalimbali walitoa maoni yao wakimsihi Rais Samia Suluhu Hassan amwachie, bila kujua kuwa Rais hana mamlaka yoyote ya kumwachia mtu ambaye anashtakiwa," alisema. "Kusonga mbele kwa kesi kama hii ambayo kwa kweli haina kichwa wala miguu imeonekana iondolewe mahakamani," aliongeza.

Alipoulizwa kama Mbowe na wenzake wanaweza kudai fidia kwa kukaa rumande kwa muda mrefu, alisema hakuna hukumu ambayo inasema hakuna hatia.

"Kama ikitokea mtu akapata hukumu inayomwambia hana hatia anaweza kudai fidia zake. Kinachotakiwa tuweke mfumo wa haki jinai unaozingatia na kusheshimu utu wa watu, usiobagua au kumuonea mtu ili mwenye makosa ndiye akamatwe na ashitakiwe na vyema kuwapo na ushahidi wa kutosha wa kumpeleka mtu mahakamani," alisema Wakili huyo. Alisema polisi na watu wengine wanaohusika watambue kwamba wanavyoingilia uhuru wa mtu wanapoka sehemu ya uhai wake kwa maana hiyo mfumo huo wa jinai uweze kufumuliwa upya.

"Mtu anaposhtakiwa kuwapo na sababu ya msingi inayoonyesha kweli kulikuwa na sababu ya kumshtaki na kuwapo na haki ya dhamana. Makosa yote yadhaminike, yakidhaminika angalau yanapunguza ile adhabu ya kupoka uhuru wa mtu kwa maana hiyo kunakuwa na jamii inayoheshimu utu wa watu," alisema Dk. Nshala.

**LHRC YANENA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema kuachiwa kwa Mbowe na wenzake ni jambo la heri.

"Maoni yangu, sheria ibadilike mtu asikamatwe kwanza halafu ndiyo muanze uchunguzi. Inakuwa humtendei mtu haki, ufanyike upelelezi kisha mtu ndipo akamatwe, tusiweke watu gerezani ambao hawana hatia," alisema.

**TEF YAPONGEZA**

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alimpongeza Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa kufuta kesi iliyokuwa ikimkabili Mbowe na wenzake huku akisema ni uamuzi sahihi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika ofisi za TEF jijini Dar es Salaam, alisema kesi ya ugaidi iliyokuwa ikimkabili mwenyekiti huyo na wenzake haikuwa na mashiko wala maslahi kwa nchi huku akidai kwamba ilikuwa ikilitia doa taifa.

■**Imeandaliwa na Maulid Mmbaga na Mary Geofrey**


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

### TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala-Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala-Lugala na Nala-Segu kuwa muda wao wa kulipia viwanja hivyo umeisha. Aidha, katika kuwawezesha kukamilisha malipo hayo, amewaongezea muda hadi tarehe 27.03.2022.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, viwanja ambavyo vitakuwa bado vinadaiwa vitarudishwa sokoni ili wateja wengine wavinunue bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji, DODOMA**

216731401

HABARI KITAIFA

# Comoro yatangaza maombolezo ajali ndege iliyoanguka baharini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI watu 12 raia wa Comoro na marubani wawili raia wa Tanzania waliopata ajali ya ndege nchini Comoro Febuari 26, mwaka huu, bado miili yao ikiwa haijapatikana na juhudi za kuwatafuta zikiendelea, Comoro imetangaza siku tatu za maombolezo.

Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Silima Ame Pereira, alisema jana kuwa serikali ya nchi hiyo imetangaza bendera kupepea nusu mlingoti kwa muda huo.

Alisema ndege hiyo ilianguka katika kisiwa cha Mwale nchini Comoro na ilikuwa ikifanya safari zake ndani ya nchi hiyo.

"Juhudi za kuitafuta ndege iliyoanguka ikiwa na abiria 12 na marubani wawili zinaendelea lakini uwezekano wa kuwapata wakiwa hai ni mdogo sana na tayari baadhi ya mabaki ya ndege hiyo yameshapatikana," alisema.

Alisema hatua hiyo imeifanya serikali ya Comoro kutangaza siku tatu za maombolezo kutokana na msiba huo mkubwa na kwamba bendera zitapepea nusu mlingoti hadi kesho.

"Serikali ya Comoro imetangaza siku tatu za maombolezo kuhusiana na msiba huo ambapo bendera zitapepea nusu mlingoti ingawa juhudi za kutafuta ndege hiyo zinaendelea," alisema.

Abiria waliokuwamo katika ndege hiyo 5H-MZA ambayo ilisajiliwa Zanzibar na inamilikiwa na kampuni ya Air Fly ilikuwa ni wanaume saba, wanawake wanne na mtoto mmoja.

Majina ya abiria hao ni Youssouf Abdoulwahad, Marzouk Ali Soilihi, Ramadhan Ahamada, Abdel Ahamed, Moustakima Avais, Moustakima Jade, Chaharizadi Soudjan, Mointoiwila Ali, Kassim Toiliha,Andjilane Mchamcd na Ali Moussa.

Marubani wa ndege hiyo ni Adil Sultan Khamis na Ashraf Abdallah Sadala Mabodi ambao ni Wazanzibari na ndege hiyo ilikodishwa nchini Comoro.

**SMZ YATOA POLE**

Kutokana na msiba huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, ametoa salamu za pole kwa ajali hiyo ambayo imepoteza raia wa Comoro pamoja na marubani wawili wenyeji wa Zanzibar.

"Rais wa Zanzibar ametuma salamu za pole kwa serikali na wananchi wa Comoro kutokana na ajali hiyo na kuwaomba ndugu na familia wawe na moyo wa subira huku juhudi zingine zikiendelea," alisema.

Familia na wazazi wa marubani wawili kutoka Zanzibar waliopata ajali hiyo, wako nchini Comoro kwa wiki moja sasa wakifuatilia kwa karibu juhudi za kutafuta watu hao, akiwamo Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Abdallah Juma Sadala, ambaye mmoja ya marubani hao ni mtoto wake.



Ofisa Elimu wa Kata ya Makumbusho, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, Simon Milobo (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Makumbusho, alipotembelea juzi, ili kuhamasisha uanzishwaji wa klabu za wanafunzi za kupambana na ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgomo wa madereva daladala watikisa

**Na Samson Chacha ,** TARIME

ZAIDI ya madereva 200 wa magari madogo ya abiria, maarufu kamadaladala na hiace, yanayofanya safari kati ya Tarime na maeneo mbalimbali jana waligoma kwa saa nne wakipinga kuhamishiwa katika stendi mpya. Madereva hao wa mabasi ya kutoka Tarime mjini kwenda Nyamongo, Sirari, Shirati, Nyamwaga, Kibuyi, Mriba, Kogaja,

Ikoma na Kinesi, walifanya mgomo huo wakitaka kupatikana suluhu ya kuhamishiwa stendi mpya ya Rebu.

Mgomo huo ulianza saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana na kuendesha magari yao hadi ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya ya Tarime Mjini kutaka suluhu ya jambo hilo ipatikane.

Wakizungumza katika kikao cha pamoja katika ukumbi wa CCM Wilaya kilichoongozwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime, Valentine Maganga, walisema stendi ya mjini Tarime ni kubwa lakini haina mpangilio mzuri wa magari.

Walisema katika stendi hiyo kuna wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga, wamejaza bidhaa, hivyo kusababisha msongamano wa magari sehemu moja.

"Tunaomba machinga waondolewe stendi ya magari ili kuegesha magari kwa ajili ya kulipa ushuru. Madereva wote wa magari madogo ya abiria, tuwekeane kanuni za kuwadhibiti madereva wenzetu ambao hawaingii stendi na kupakilia abiria nje, hivyo kuikosesha halmashauri mapato kwa kutofuata taratibu,

"Stendi ya Gamasara ambayo mabasi makubwa yangeweza kwenda bado haijakamilika. Tunaomba kwa wakati huu tuendelee kuwapo stendi ya mjini hadi pale mwafaka utakapopatikana," walisema viongozi wa madereva hao, Joseph Kazimoto, Masubo Nkori na Yakob Marwa kwa nyakati tofauti.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, alisema madereva hao wanapaswa kuhamia stendi mpya ya Rebu kwa kuwa lengo la kufanya hivyo ni kupanua mji badala ya kuwa na stendi moja ambayo ina mlundikano wa magari.

Pia alisema kutumika kwa stendi moja kunasababisha ukusanyaji ushuru kuwa mgumu kutokana na madereva wenye magari madogo kuegesha nje ya stendi na kukosesha halmashauri mapato.

"Madai yao tumeyasikia ila tunawaomba waendelee kutoa huduma kwa wasafiri huku tukijadiliana na viongozi wenzetu wa serikali, chama na halmashauri," alisema Kamote. Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime, Valentine Mganga, alisema chama kiko tayari kusikiliza malalamiko ya madereva hao na kusisitiza halmashauri kuitisha kikao cha pamoja na wenye magari madogo madereva ili kupata mwafaka kwa pande zote mbili.

"Chama tunashauri halmashauri kukaa pamoja na madereva ili kupata mwafaka. Kwa sasa waendelee kuwapo katika stendi hiyo hadi suala hili litakapopatiwa ufumbuzi, madereva nendeni mwendelee kutoa huduma kwa wananchi kwanimgomo huu hauna faida kwa pande zote mbili, kwenu madereva na halmashauri," alisema Maganga.

## Serikali kuongeza uzalishaji umeme

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imesema inajipanga kuongeza uzalishaji wa umeme nchini na kudhibiti matumizi ya nishati hiyo ili kukidhi mahitaji ya uwekezaji mkubwa.

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati, Edward Ishengoma, aliyasema hayo jana kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Felchesmi Mramba, alipozindua mradi wa utekelezaji wa matumizi bora ya nishati unaotekelezwa na wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Umoja wa Ulaya (EU) mjini hapa jana.

Alibainisha kuwa utafiti uliofanywa kuhusu matumizi ya umeme nchini, umebaini umeme mwingi unatumika majira ya saa mbili usiku kutokana na muda huo kuwa na watumiaji wengi wa umeme, vikiwamo viwanda.

"Hapa nchini matumizi ya juu kabisa ambayo hayajawahi kutokea, yalitokea Novemba mwaka jana ambayo ni megawati 1,307," alisema.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa taifa kwa sababu utaongeza nishati na kupunguza matumizi yasiyo rafiki ya nishati nchini.

Ishengoma alisema matumizi bora ya nishati ni chanzo kizuri cha nishati katika nishati ile ile unayoitumia na kwamba upo uwezekano wa wanaotumia nishati ya umeme mkubwa kutumika kwa nusu yake.

"Kwa mfano, katika hayo matumizi ya juu kabisa kutokea yalitokea mwezi Novemba megawati 1,307, nishati ikitumika vizuri kwa matumizi mazuri wataalamu wanasema unaokoa asilimia 20 ya megawati hizo ambayo ni megawati 261," alifafanua.

Alisema mradi huo ni utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka 2015 baada ya kufanya maandalizi mbalimbali ikiwamo utafiti kwenye viwanda, majengo makubwa ya serikali, miundombinu ya maji ili kuona wanapoteza umeme kiasi gani na katika maeneo yapi.

Mtaalamu wa Miradi wa UNDP, Abasi Kitogo, alisema mradi huo unaogharimu Sh. bilioni 22.9 utasaidia nchi na dunia kufikia malengo ya kupata umeme au nishati bora, umeme jadidifu na kuwa na matumizi bora ya nishati.

Meneja Miradi ya Nishati wa EU, Francis Songela, alisema wanaamini matokeo ya mradi huo yatasaidia kutanua zaidi uhamasishaji matumizi ya nishati kwa njia bora.

Songela alisema wadau wa mradi watajengewa uwezo kielimu na vifaa na kuwa na waatalamu wengi ambao watashiriki katika sekta mbalimbali ikiwamo majengo, viwanda na katika kaya ambazo nishati ndiyo imekuwa kitu cha msingi zaidi.

Akizungumza kwa niaba ya taasisi zisizo za kiserikali, Mkurugenzi wa Program kutoka taasisi ya kijamii inayoshughulika na masuala ya nishati, mabadiliko ya tabianchi na mazingira, Eusta Kibona, alisema mradi huo ni muhimu kwa jamii kwa kuwa unakwenda kupunguza matumizi ya nishati na kiasi kikubwa cha fedha kilichotumika kwa ajili ya nishati, kitatumika kwenye mambo mengine ya maendeleo.

## Amuua mke wake kisha kujinyonga

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MWANAMUME aliyejulikana kwa jina la Anicet John (32) anadaiwa kumuua mke wake Jeniviva Timotheo (29) kwa kumkata na panga shingoni kisha kujinyonga kwa kutumia chandarua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame Hamad, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 2, mwaka huu, katika Kijiji cha Mtakuja, Wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

Alisema John alifunga mlango wa chumba chao kisha kumuua mke wake na baada ya kutekeleza mauaji hayo, naye alijinyonga kwa chandarua alichokifunga kwenye kenchi chumbani kwake.

Kamanda Hamad alisema chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa kifamilia unaohusishwa na wivu wa mapenzi na kwamba mke alikuwa akimtuhumu mumewe kuwa na wanawake wengine nje (michepuko) hali ambayo ilikuwa ikisababisha mgogoro kila mara ndani ya nyumba.

Kwa mujibu wa Kamanda Hamad, John kabla ya kujinyonga, aliandika ujumbe unaosomeka kuwa: "Nimejinyonga kwa hiari yangu mwenyewe" na kwamba mpaka sasa hakuna mtu aliyekamatwa wala kuhusishwa na tukio hilo.

Hamad alisema miili ya marehemu imefanyiwa uchunguzi na kisha kukabidhiwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi.

# Afungwa jela maisha kwa kubaka mtoto

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kahama Mkoani Shinyanga, juzi ilimhukumu Jackson Burton (19) mkazi wa Kagongwa, Manispaa ya Kahama kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na kosa la kumbaka mtoto wa miaka mwili.

Mtuhumiwa alidaiwa alifanya kitendo hicho eneo la Kagongwa kwa kumbaka mtoto huyo (jina linahifadhiwa) na kumsababishia maumivu makali sehemu za siri.

Mwendesha Mashitaka, Evodia Baimo, aliiambia mahakama kuwa Burton alifanya kitendo hicho Julai 17, mwaka jana katika kata ya Kagongwa baada ya kumkuta mtoto huyo akicheza nyumbani na kumpeleka chooni na kufanikisha kitendo hicho ovu.

Alidai kuwa mashahidi katika kesi hiyo walikuwa wanne akiwamo mama mzazi wa mtoto huyo, ambaye katika ushahidi wake alidai kuwa siku hiyo aliondoka kwenda zahanati kupata matibabu na aliporudi nyumbani alimkuta mtoto na kumweleza kuwa amefanyiwa kitendo hicho na mtuhumiwa.

Shahidi huyo aliendelea kuiambia mahakama kuwa baada ya kumkagua mwanawe, alimkuta akiwa na majeraha sehemu zake za siri hali iliyotokana na kuingiliwa na mshitakiwa huyo kwa nguvu.

Shahidi namba mbili ambaye alikuwa balozi wa mtaa, alidai kuwa baada ya kuletewa taarifa za tukio hilo, aliamua kupeleka malalamiko hayo hadi kituo cha polisi ambako yalifanyiwa kazi.

Naye mtoto aliyetendewa kitendo hicho, alidai kuwa mshitakiwa alimkuta akiwa ameekaa nje ya nyumba peke yake na baadaye alimchukua na kumpeleka chooni na kumbaka na kusikia maumivu makali kabla ya kumweleza mama yake.

Pia mtoto huyo alimtambua mshitakiwa huyo mahakamani kuwa ndiye aliyemfanyia kitendo hicho kabla ya shahidi mwingine, Dk. John Marwa kutoka Zahanati ya Kagongwa aliyemfanyia uchunguzi mtoto huyo na kumkuta akiwa amevimba sehemu zake za siri na kitu bapa kikiwa kimeingia ukeni mwake kwa kulazimishwa.

Upande wa utetezi uliiambia mahakama kuwa hakufanya kitendo hicho kwa kuwa yeye alikuwa akitoka nyumbani kwake asubuhi na kurudi jioni na pia hawezi kufanya kitendo hicho kwa mtoto kwa kuwa bado ni mdogo sana kwake na tayari alikuwa ameathirika na Ukimwi.

Hata hivyo Hakimu Mkazi Christina Chovenye, alisema ameridhika na ushahidi uliotolewa, hivyo kumtia hatiani mshitakiwa huyo na kumhukumu kifungo cha maisha jela kwa kuwa makosa kama hayo yako mengi na yamekuwa yakiongezeka kila uchao.

Kabla ya hukumu, Baimo aliiomba mahakama kutokana na kosa alilolifanya mshtakiwa kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia kama hiyo ya ubakaji huku upande wa mshtakiwa akiomba apunguziwe adhabu kwa kuwa bibi yake anamtegemea na yeye ni kijana mdogo.

## TEA, BRAC zasaidia kompyuta shule

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na asasi ya BRAC-Maendeleo, imetoa kompyuta 120 zenye thamani ya Sh. milioni 132 kwa shule tatu za wilaya ya Temeke kwenye mradi wa "Skills for Their Future".

Kompyuta hizo zilikabidhiwa na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, kwenye hafla iliyofanyika jana katika Shule ya Sekondari Karibuni iliyoko Chang'ombe, Dar es Salaam. Shule zilizonufaika na msaada huo ni Miburani, Wailes na Karibuni.

Akizungumza kwenye tukio hilo, Jokate alisema makubaliano baina ya BRAC - Maendeleo Tanzania na TEA ni mfano wa namna taasisi za umma na zile zisizo za kiserikali au binafsi zinavyoweza kufanya kazi kwa pamoja katika kuboresha maisha ya wananchi.

Jokate alisema TEA inafadhili ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwa ni pamoja na vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo, mabweni, mabwalo na majiko yake, maabara na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu Tanzania Bara na ngazi ya elimu ya juu kwa Zanzibar.

"Nichukue nafasi hii kuwasilisha shukrani za dhati kwa serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania chini ya Mkurugenzi Mkuu, Bahati Geuzye. Temeke ni miongoni mwa Wilaya zinazonufaika na Miradi inayofadhiliwa na TEA," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye alisema mamlaka hiyo imeshakarabati shule kongwe 17 za sekondari kati ya 89 zilizopo katika mpango huo wa ukarabati na hivi karibuni ilishiriki kukarabati shule nne za msingi mkoani Dodoma.

Alisema kutolewa kwa kompyuta hizo ni uzinduzi wa mradi wa 'Skills for Their Future' unaolenga kutoa mafunzo ya kidijitali kwa vijana wa shule za sekondari ili kuwawezesha kupata ujuzi na stadi zitakazosaidia kuboresha maisha yao.

"Kompyuta hizi zinatolewa baada ya kusainiwa kwa makubaliano maalum ya ushirikiano baina ya TEA na BRAC-Maendeleo ikiwa ni mkakati wa kuunga mkono serikali wanafunzi kujifunza kupitia TEHAMA (teknolojia ya habari na mawasiliano) katika ngazi zote za elimu nchini," alisema.

Alisema kompyuta hizo zitanufaisha wanafunzi 1,800 na walimu 45 na kwamba ni matumaini yao kwamba wanafunzi wa shule hizo tatu watatumia vizuri fursa ya miundombinu hiyo ya kompyuta kupata maarifa na taaluma zitakazowawezesha kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Alisema walimu nao watatumia fursa hiyo kuboresha ufundishaji wa masomo na hivyo kusaidia shule zao kufanya vizuri kitaaluma na kwamba TEA inafarijika kuona wadau wa maendeleo kama BRAC wanatoa mchango wao kupitia mamlaka ya elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa BRAC-Maendeleo, Suzan Bipa, alisema asasi hiyo imeichagua wilaya ya Temeke katika kutekeleza miradi mbalimbali na wameshirikiana na wilaya kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu.

"Tunawashukuru viongozi wa wilaya hii kila tunapokuja kuanzisha mradi mpya mnatupokea vizuri na mnatupa ushirikiano mkubwa nawapongeza sana na tunafanya hivi kwenye maeneo mengi nchini," alisema.

Alisema mbali na mradi huo wanatekeleza miradi mingine ya usalama na chakula uwezeshaji kwa vijana na wanawake na katika mradi huo wamefanya mambo mengi wilaya ya Temeke.


**NAMBA YA USAJILI 4152**
**WANAOIDAI NCU (1984) LTD.**

1. NCU (1984) Ltd. imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 Ni Chama Kikuu cha Ushirika cha walimaji wadogo wa zao la Pamba Jijini Mwanza katika Wilaya za Sengerema, Magu, Misungwi, Ukerewe na Kwimba.

2. NCU (1984) Ltd. inafanya mapitio ya madeni yake mbalimbali yakiwemo ya wazabuni ama watu waliofanya biashara na kutoa huduma kwa Chama hiki hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020. Madeni yanayohusu tangazo hili sio ya Vyama vya Msingi (AMCOS) Wanachama wetu ambao utaratibu wa kuendelea kuyahakiki unaendelea wala haihusu watumishi waliopo kazini au ambao ajira zao zimeshakoma, Kwa kuwa makundi haya utaratibu wao unaendelea kufanyiwa kazi.

**Namna ya kuwasilisha taarifa za madeni;**

a. Wadai wote ambao walifanya biashara ama kutoa huduma kwa Chama hiki hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 wawasilishe nyaraka zao za madai katika Ofisi ya Chama, iliyopo jengo la NCU (1984) Ltd. katika chumba na 102 iliyopo ghorofa ya kwanza katika Ofisi ya Meneja Mkuu.
b. Kila mdai awe na uthibitisho kutoka mamlaka sahihi ya NCU (1984) Ltd. ya bidhaa/huduma hiyo aliyofanya ikiambatana na uthibitisho wa kupokelewa kwa bidhaa/huduma hiyo.
c. Ikibainika mleta taarifa amewasilisha nyaraka ama taarifa za uongo/kugushi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.
d. Taarifa zinazowasilishwa ziwe zimethibitishwa na mwanasheria ambaye ni wakili kwa kuwekwa saini na kugongwa muhuri wa wakili. Hatutapokea wala kufanyia kazi taarifa ya madai ambayo haijapata uthibitisho huu muhimu.
e. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha nyaraka za madai iwe kabla au ifikapo siku ya Ijumaa tarehe 11 April 2022 saa 10:00 (Kumi Kamili) jioni.
f. Kila anewasilisha taarifa zake ahakikishe anaweka saini kwenye karatasi maalum iliyoandaliwa kwa zoezi hili ili kuthibitisha muitikio wake.

Baada ya zoezi la kupokea nyaraka kuhitimishwa, zitafanyiwa kazi na kila mhusika atafahamishwa matokeo ya taarifa zake pindi uhakiki na ufuatiliaji utakapokamilika. Aidha naomba ieleweke kwamba wakati wa uwasilishaji nyaraka za madai sio muda wa kufanya mazungumzo wala uhakiki wa taarifa za mdai.

**Anuani;**
**MENEJA MKUU,**
**NCU (1984) LTD,**
**JENGO LA NCU (1984) LTD. MAKAO MAKUU, CHUMBA NA. 102 GHF YA 1, KITALU NA……, BARABARA YA KENYATA MKABALA NA CRDB BANK,**
**S. L. P. 09, MWANZA.**
**BARUA PEPE; info@ncultd.or.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Juhudi zatakiwa kulibeba soka la wanawake nchini

**WAKATI** Simba ikiwa ndio klabu pekee hapa nchini imebakia ikipeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Timu ya Taifa ya Soka ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 kesho inakabiliwa na kibarua dhidi ya wenzao kutoka Botswana.

Wawakilishi hao wa Tanzania watawavaa Botswana kuanzia saa 10:00 kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar, ni katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za U-17, zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini India.

Timu hizo zitarudiana kati ya Machi 17 na 19, mwaka huu jijini Gaborone na mshindi wa jumla atakutana na kati ya Burundi au Cameroon.

Ni historia isiyofichika kuwa katika kipindi cha miaka 10, timu za taifa za wanawake zimeleta makombe mbalimbali hapa nchini na kuwazidi kaka zao.

Lakini mbali na mafanikio hayo, timu zote za taifa za wanawake ukianza na hii ya U-17, Tanzanite Queens (U-20) na ile ya wakubwa, Twiga Stars, zote zimekosa udhamini.

Mabosi wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), mara kwa mara wamewakaribisha wadhamini kuwekeza katika timu hizo kwa sababu wanaamini endapo nguvu za ziada zitapatikana, basi wanaamini kukosekana udhamini isiwe kikwazo kwa sababu wanaamini ndoto za Tanzania kupeperusha bendera yake fainali za dunia ni rahisi kupitia soka la wanawake.

Umefika wakati makampuni yakaona fahari kudhamini au kuwekeza kupitia mpira wa miguu wa wanawake na hakika kile ambacho watakitoa, kitarejea zaidi lakini wakifurahia mafanikio ambayo yatapatikana kupitia mchango wao wa kusaidia kulipia gharama maandalizi ya timu.

TFF imekuwa ikipambana kuhakikisha timu hizo za wanawake zinakaa kambini kwa wakati, zinapata vifaa lakini ikipambana kuwapa posho wachezaji kwa ajili ya kuwaongezea morali ya kufanya vizuri katika kila mashindano wanayoshiriki.

Tunazikumbusha kampuni na taasisi mbalimbali kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan kuwekeza kwenye michezo kuanzia kwenye maandalizi ya timu ili kusubiri matokeo chanya kwa sababu anaamini ili bendera ya nchi ipepee vyema, ni lazima timu au wanamichezo husika wawe walipata maandalizi yanayostahili.

Tunaamini kwa kuwekeza vyema katika kuanzia katika maandalizi ya awali, basi kupata matokeo chanya ndio jambo linalotarajiwa na si kusubiri hadi timu itakapofuzu, ndipo zawadi mbalimbali kuanza kutolewa.

Tuwaamini wasichana au wanawake, kwa sababu njia ya wao kukata tiketi ya kushiriki fainali za dunia ni fupi ukilinganisha na timu za wanaume, lakini ili yote hayo yafanikiwe, fedha na huduma mbalimbali muhimu zinahitajika na hakuna mwingine ambaye anasubiriwa kuwashika mkono U-17 ambao kesho wanakibarua kizito nyumbani na baadaye kurudiana na wapinzani wao huko ugenini Gaborone.

Endapo wadhamini watajitokeza, basi timu hizo zitafanikiwa kupata mechi za kirafiki za kimataifa na michezo hiyo itasaidia kuwajenga wachezaji badala ya sasa ambapo wanajipima na timu za wanaume kabla ya kucheza mechi zao za mashindano.

TFF imefungua milango kwa kampuni na taasisi kujitokeza kusaidia timu hizo kwa sababu inaamini nguvu za pamoja zitasaidia kuifanya ndoto ya kucheza Kombe la Dunia inatimia na kila aliyestahili kupongezwa atapata heshima yake.

Tukumbuke mafanikio katika mpira wa miguu yanatokana na uwekezaji unaostahili na kamwe hakuna miujiza au fita za nje ya uwanja. Timu inayopata maandalizi mazuri ndiyo yenye nafasi ya kufanya vyema na si vinginevyo.

Mungu ibariki Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17. Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la Mshery, fundisho klabu kutosajili kizamani

**NAKUMBUKA** miaka mingi nyuma, mzee mmoja ambaye nina undugu naye, mkazi wa Tabata alimwita kijana wake na kumpa eneo la uwanja nyuma ya nyumba yake na kumtaka ajenge.

Wakati huo eneo hilo lilikuwa bado baadhi ya maeneo bado mapori. Ilikuwa haijachangamka kama ilivyo sasa. Kijana akakataa na kumwambia baba yake hawezi kuchukua eneo hilo hivi hivi bila ya kuandikishiana. Mzee huyo alikasirika na kumuuliza ina maana hamwamini yeye baba yake, anaogopa nini kuja kumgeuka?

Kijana akamjibu baba yake kuwa dunia ya sasa siyo kama ile ya zamani walioishi wao ambapo watu walikuwa na utu, kuheshimiana, pamoja na uaminifu uliopitiliza.

Akamwambia tatizo siyo yeye, ila wadogo zake ambao bado wadogo wakiwa wakubwa na kugundua kuwa alipewa eneo la uwanja bila maandishi, inaweza kumletea matatizo. Kwa shingo upande mzee akakubali kuandikishana na kijana wake.

Miaka ikaenda, mzee akaanza kuugua. Kabla hata hajafa, alishuhudia mgogoro au ugomvi kwa kijana wake mkubwa dhidi ya wadogo zake, wakidai eneo alilojenga nyumba ni la familia, na baba yao alimpa kwa mdomo bila maandishi yoyote.

Kabla ya kufariki, mzee aliwaita wote na akawaonyesha nyaraka zote zinazoonyesha waliandikishiana na hakumpa kwa maneno. Ndipo watoto hao walipoamini na kutulia. Baada ya muda mzee akafariki.

Kisa hiki kifupi nimekitoa hapa kuonyesha imefikia wakati dunia ya sasa hata wanandugu wenyewe hawaaminiani na wanageukana, achilia mbali watu baki.

Miaka ya nyuma walikuwa wakiishi kwa kuaminiana, na walikuwa waminifu.

Mtu anaweza kumpa mwenzake kitu cha thamani na asimgeuke. Wengi walikuwa wanawashangaa wazungu au watu wa nje kila kitu wanafanya kazi ya kuandikishiana. Kumbe wao walishatoka zamani kwenye maisha yale. Waliyaishi zamani na wakawa wameingia kwenye maisha ya kila mmoja kujitazama yeye. Maisha ya ubinafsi. Ndiyo maana kwa sasa kila kitu kinakwenda kwenye maandishi na mikataba. Hata kwa mtu ambaye unayemwamini kupita kiasi.

Majuzi kuliibuka taarifa za klabu ya Mtibwa Sugar kulalamika kutolipwa fedha zake za usajili kwa ajili ya aliyekuwa mchezaji wao golikipa, Aboutwalib Mshery. Kupitia kwa msemaji wao, Thobias Kifaru alisema walikuwa hawajapewa malipo yao, licha ya kwamba walisaini kukubali mchezaji huyo aondoke.

Hapa ndipo niliposhangaa sana. Hivi hadi leo karne hii, bado kuna klabu inauza mchezaji kwa mali kauli?

Na sidhani kama Mtibwa Sugar waliweka kipengele wasipolipwa fedha hiyo hadi siku fulani basi mkataba huo utakuwa batili, au watakuwa wakiuka kanuni.

Sifikiri kama waliweka kwa sababu kama ni hivyo, wala wasingekuwa na tabu ya kupiga kelele katika vyombo vya habari.

Kilichotokea tu ni kwamba Mtibwa Suagr iliamua kupiga kelele ili kuonewa huruma, au kuifanya Yanga ione aibu na kulipa fedha hiyo ya usajili.

Kwanza nilishangaa kwa klabu kubwa kama Yanga ambayo ilikuwa na uhitaji zaidi wa mchezaji kutoipa Mtibwa Sugar pesa za kipa huyo, kwani kipa wake Djigui Diara alikuwa amekwenda Cameroon kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2022), lakini mshangao wangu zaidi ni pale Wakatamiwa hao kushindwa kutumia fursa hiyo kupiga pesa ya haraka na badala yake wakamtoa kwa mali kauli, wakati wao wenyewe wanamhitaji.

Dunia ya leo, si kwenye soka, au maisha ya kawaida, hakuna kitu kama hicho, watu kwa sasa hawaaminiani. Hakuna maisha ya kijamaa tena kama yale ya zamani.

Kama hamkuandikishana, mtu anaweza kukuruka hivi hivi huku anakujua, na ushahidi kukawa hakuna.

Kwa hili lililotokea, liwe funzo kwa klabu zote nchini. biashara ya wachezaji ndiyo kubwa zaidi kwa klabu zote dunaini. Inashangaza kuona klabu inakubali mchezaji aondoke ikiwa haijalipwa chochote kile. Cha kushangaza ni kwamba hakuna maandishi yoyote yanayowafunga waliomchukua.

Klabu za Ligi Kuu au nyingine zisionyeshe unyonge linapokuja suala ya klabu kubwa kutaka kusajili wachezaji wao wanapokuwa kwenye mikataba kwa kukubali kila wanachoambiwa. Pigeni pesa, kama watakupa robo, nusu, au nusu na robo, andikishianeni zilizobaki zitalipwa lini na zisipolipwa nini kifanyike. Zikiendelea kufanya biashara 'kishikaji' zitaendelea kuumia au kusubiri huruma ya kelele za waandishi wa habari na wachambuzi.

# Malori yanaswa uchotaji mchanga wa mtoni Dar

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Bonde la Wami Ruvu imefanya operesheni maalumu ya ukaguzi na kukamata malori manne kwa tuhuma za kuchukua mchanga Mto Tegeta na Mto Nyakasangwe ulioko Boko Kanisani bila kibali, uharibifu wa mazingira na kuhatarisha usalama wa mito na makazi ya watu.

Akizungumza katika operesheni hiyo jana katika Mto Tegeta, Kaimu Ofisa wa Bonde hilo Dar es Salaam, Halima Faraji, alisema uchimbaji mchanga una utaratibu maalumu na aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, alitoa maelekezo na mwongozo wa kuundwa kikosi kazi cha usimamizi wa shughuli za usafishaji mito Dar es Salaam.

Alisema kikosi kazi hicho kinawahusisha Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Ofisi ya Makamu wa Rais, Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu, Tume ya Madini, TANROADS, TARURA, DAWASA, vyombo vya ulinzi na usalama na halmashauri zote za Dar es Salaam.

"Kwa sasa mito yote haina vibali isipokuwa Mto Msimbazi ambao kuna makandarasi wanaendelea na kazi pamoja na vijana wachache kwenye maeneo maalumu yaliyochaguliwa," alisema.

Aliongeza kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wanaochimba mchanga ambao wanaingia kusafisha mito bila kupewa idhini na serikali na wanachukua mchanga kwa kiwango kikubwa na kuharibu mazingira.

"Tumefanya operesheni kwa siku mbili katika baadhi ya mito ya Dar es Salaam, lengo ni kuhakikisha mito yetu inakuwa salama, lazima itiririshe maji vizuri kuelekea baharini, lakini vijana wetu wanachokifanya ni kuharibu mito kwa kufanya bila utaratibu na malekezo ya wataalamu.

"Waache kuharibu mito, waache kuharibu mazingira, mito inatakiwa kutunzwa, rasilimali za maji zinatakiwa kutunzwa na jukumu la kulinda vyanzo vya maji siyo la bonde pekee yake au taasisi nyingine, ni jukumu la kila mwananchi," alisema Halima.

Alitoa Rai kwa wananchi wanaokaa karibu na mito, wanapoona watu wanaochimba mchanga, watoe taarifa kwenye serikali za mitaa au kwa maofisa wa bonde hilo.

Alisema viongozi wa serikali za mitaa wanatakiwa kuwajibika kwenye suala hilo kwa kuwa wana jukumu la kusimamia mikataba inayotolewa na serikali ya kusafisha mito kwa kuwa miongozo iliyopo isipofuatwa, uchimbaji wa mito utakuwa



Ofisa Mradi, Usawa wa Kijinsia wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Enrica Hofer (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kwenye warsha ya waandishi wa habari, kuhusu uelewa wa haki za wanawake, ilioandaliwa na shirika hilo kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Kulia ni Mtaalam wa Usawa wa Kijinsia wa shirika hilo Sizarina Hamis na mwandishi David Mayunga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# NSSF yachangia vifaa tiba hospitalini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umetoa msaada wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Zanzibar kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani.

Vifaa tiba hivyo ni vitanda vya kujifungulia na mashine za kupima shinikizo la damu vilivyokabidhiwa na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, kwa Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Msafiri Marijani.

Lulu alisema mfuko huo ulitoa msaada huyo kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka Machi 8, ikiwa na kaulimbiu isemayo 'Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu'.

Akipokea msaada huo, Dk. Marijani alisema kwa niaba ya uongozi wa hospitali hiyo na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, wanaishukuru NSSF kwa kutoa vifaa tiba hivyo ambavyo vitatumika katika kuokoa maisha ya wananchi wanaokwenda kupata huduma.

Dk. Marijani alisema wamepokea msaada huo kipindi ambacho mahitaji ya vifaa tiba katika hospitali hiyo ni makubwa licha ya serikali kujitahidi kununua vifaa vya kutolea huduma.

"Tunawashukuru NSSF kwa kutupatia msaada huu ambao unaenda kusaidia kuokoa maisha ya wagonjwa wanaopata huduma katika hospitali yetu, nina wahakikishia kuwa vifaa hivi vitatumika kwa lengo lililokusudiwa," alisema.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu, alisema kuwa baada ya kupata uhitaji wa vifaa tiba kutoka kwa uongozi wa hospitali hiyo, mfuko uliamua kuwaunga mkono kwa kutoa vifaa hivyo ambavyo vitasaidia katika kuokoa maisha ya wagonjwa.

"NSSF kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu tunaendelea kuwashukuru wenzetu wa ZSSF (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar) kwa kuzidi kukuza ushirikiano baina ya mifuko hii pamoja na Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kukubali kupokea vifaa tiba hivi ambavyo vitatumika kuwahudumia wagonjwa mbalimbali," alisema.

Lulu alisema mfuko pamoja na kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwamo kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao pia unachangia shughuli mbalimbali kwa manufaa ya Watanzania na taifa kwa ujumla kwa kuwajibika katika jamii (CSR) hasa katika maeneo ya afya, elimu, michezo, jamii na kudhamini shughuli mbalimbali za wadau.

Mwenyekiti wa Wanawake NSSF, Vaileth Segeja, alisema wametoa msaada huo kwa sababu mfuko una sera ya kutoa misaada katika jamii na kutoa wito kwa wanawake wote waliopo katika sekta isiyo rasmi kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii ikiwamo NSSF na ZSSF kwa ajili ya maisha yao ya sasa na baadaye.

Nassor Hassan, Ofisa Utawala wa ZSSF, alisema kazi kubwa ya mifuko ya hifadhi ya jamii ni kuihifadhi jamii pale inapopata janga ikiwamo ugonjwa na ndio maana NSSF iliamua kutoa msaada wa vifaa tiba hivyo ili vikasaidie kuokoa maisha ya wananchi.

Alisema NSSF na ZSSF wana ushirikiano wa muda mrefu katika kusaidia baadhi ya shughuli kama kuhakiki wanachama na kwamba wataendelea kushirikiana kwa mustakabali wa taifa na jamii kwa ujumla.

# Wilaya zanufaika mradi wa mtama

**Na Faustine Feliciane,** BAHI

WAKULIMA wa mtama katika wilaya sita za Mkoa wa Dodoma wamenufaika na mradi wa kilimo himilivu cha zao hilo (CSA) unaosimamiwa na Shirika la Farm Africa na kuwezeshwa na Shirika la Chakula Duniani (WFP).

Kwa mujibu wa WFP, kupitia mradi huo wakulima hao katika msimu wa mwaka 2020/21 wamevuna tani 28,000 za mtana uliowaingizia Sh. bilioni 13.5.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Dodoma, Mkuu wa Ofisi Ndogo ya WFP iliyopo jijini hapa, Neema Sitta, alisema mradi huo umeleta tija kubwa kwa wakulima ambao kwa sasa mbali ya kuvuna mtama mwingi, pia wamekuwa na soko la uhakika.

"Mradi wa CSA unatekelezwa katika vijiji zaidi ya 200 vilivyopo kwenye wilaya sita za Mpwapwa, Chamwino, Bahi, Kongwa, Chemba na Kondoa ambapo kwa msimu wa mwaka 2020 hadi 2021 wamefanikiwa kuuza zaidi ya tani 28,000 za mtama zenye thamani ya Sh. bilioni 13.5," alisema Neema.

Aliongeza kuwa mradi huo licha ya kusimamiwa na WFP, unadhaminiwa na Shirika la Maendeleo la Ireland (IrishAid). "Mradi huu ni wa gharama ya Sh. bilioni 1.7 na umegusa wakulima zaidi ya 22,000 ambao wapo kwenye mradi kutoka katika wilaya hizo sita lakini pia umenufaisha watu 100,000 ndani ya Mkoa wa Dodoma," alisema.

Aliendelea kubainisha matarajio yao ni kuona wakulima wa mtama wanaongeza uzalishaji katika msimu huu mpya wa kilimo na WFP wako tayari kuhakikisha wanashirikiana kikamilifu na wakulima hao wa mtama.

"Tuliweka mkazo kwenye zao hili la mtama kwa sababu zao hilo linastawi kwenye ardhi na mazingira ya Dodoma pamoja na uhakika wa soko, unajua mazingira ya Dodoma ni yenye ukame na mvua kidogo," alisema.

Meneja Mradi wa Kilimo Himilivu cha Mtama kutoka Shirika la FarmAfrica Tanzania, Grace Changanyika, alisema kuwa kupitia mradi huo, wakulima wa mtama wamepiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Alisema maendeleo ya mradi huo yanatokana na kuwapo kwa soko la mtama la uhakika ambapo wanunuzi wakubwa ni pamoja na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) ambao wanaendesha kilimo cha kimkataba.

"Kuwapo kwa mnunuzi kama TBL na wengine kumefanya bei ya mtama kwa wakulima kuwa ya kuridhisha kwa sababu kwa sasa bei sokoni ni Sh. 550 kwa kilo moja, tofauti na bei ya awali ambapo mtama ulikuwa unauzwa kati ya Sh. 250 na 300 kwa kilo," alibainisha. Baadhi ya wakulima wa zao hilo wameishukuru WFP na FarmAfrica kwa kuwapelekea mradi huo ambao umewawezesha kubadili maisha yao.

Mmoja wa wakulima hao, Patrick Mbeho ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Mkola wilayani Bahi, alisema mradi huo umemletea mapinduzi makubwa kwenye maisha yake kwa kupata mafaniko makubwa.

"Kwangu haya ni mapinduzi ya kiuchumi, kijamii na maendeleo kwani nilikuwa napata Sh. milioni mbili kwa shamba la ekari 20 ila kwa sasa baada ya kuingia mradi huu na kupata elimu, napata hadi Sh. milioni sita mpaka saba, nimejenga nyumba ya biashara, nimenunua mashine ya kupembulia mtama na mengine mengi," alisifu.



Mtoa huduma wa Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, Walbarga Genes Massawe, akiwaelekeza wanafunzi wa shule ya sekondari Azania, jijini Dar es Salaam jana, namna ya kutumia huduma ya E- Fahamu inayowezesha wanafunzi kupata elimu kidijitali iliyoandaliwa na taasisi hiyo, kwa kushirikiana na African Child Projects ambayo itaunganisha shule 50 za umma zilizoko katika mikoa 10 nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 21/- kumaliza kero ya maji Songwe

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKOA wa Songwe umepanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 21 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema hayo juzi katika hafla fupi ya makabidhiano ya vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 290 kwa ajili ya mradi wa maji wa Nselewa-Mlowo wilayani Mbozi.

Alisema katika kipindi cha miezi sita tayari serikali imeupatia mkoa wa Songwe Sh. bilioni 10 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji 30 iliyopangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22.

Mgumba alisema Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Songwe umedhamiria kumaliza kero ya maji kwa kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji hadi kufikia asilimia 85.

Akihutubia wananchi katika hafla hiyo iliyofanyika katika kitongoji cha Zanzibar katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo, Mgumba alisema mradi huo utaongeza hali ya upatikanaji maji kutoka asilimia 74 hadi asilimia 85.

Naye Meneja wa RUWASA Mkoa wa Songwe, Mhandisi Charles Pambe, akizungumzia utekelezaji wa mradi huo wa maji wa Nselewa- Mlowo, alisema ni wa miezi mitatu na utagharimu Sh. milioni 501.

"Mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa nguvu kazi (Force Account) na tunatarajia ndani ya mwezi mmoja tutakuwa tumekamilisha na kuukabidhi na wananchi kuanza kupata huduma ya maji," alisema Pambe.

Pia Pambe alisema tayari RUWASA imemaliza tatizo la muda mrefu la miradi ya maji iliyojengwa kwa gharama kubwa bila kutoa maji katika mkoa huo.

Alisema Songwe ulikuwa na miradi 'kichefuchefu' katika wilaya za Momba na Songwe na yote imerekebishwa na sasa inatoa maji, huku miradi miwili kati ya minne katika wilaya ya Mbozi nayo imepatiwa ufumbuzi.

Mradi huo, alisema ukikamilika utatatua kwa kiasi kikubwa tatizo la maji katika Mamlaka ya Mji wa Mlowo na Wilaya ya Mbozi ambayo upatikanaji wa huduma hiyo ulikuwa asilimia 44 tu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Nshenye, aliwataka wananchi wilayani humo kuwa wazalendo kwa kutunza miradi ya maji amabayo serikali imetoa fedha nyingi kuitekeleza.

# DC apiga 'stop' vijana kukaa vijiweni

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa wilaya ya Mufindi mkoani Iringa. Saad Mtambule, amepiga marufuku vijana kukaa vijiweni badala yake wafanye kazi ili kujikwamua kiuchumi.

Amri hiyo aliitoa juzi wakati akizungumza na vijana 100 wanaotoka kwenye mazingira magumu kata za Ihanu, Luhunga na Mdabulo wanaoendelea na mafunzo ya afya ya akili kwenye Ukumbi wa Yatima Igoda.

Mtambule aliwataka vijana kupitia mradi ya Youth Agency Mufindi (YAM) kuunda vikundi vya kiuchumi ili kunufaika na mikopo isiyo na riba toka halmashauri badala ya kukaa Vijiweni bila kazi.

Pia mkuu huyo wa wilaya aliwataka vijana hao kuunda vikundi na wale wenye ulemavu kuungana hata wawili kuomba mkopo.

Alisema serikali ya wilaya haitapenda kuona vijana wakizurura mtaani au kushinda vijiweni bila kazi na kuwa watakaokamatwa watafikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Kuhusu mafunzo hayo, aliwataka vijana waliobahatika kuzingatia masomo hayo na kutokukatishwa tamaa na changamoto wanazokumbana nazo bali wajipe moyo na kuamini kuwa wakati wao wa kuinuka ni sasa, hivyo hawana budi kukabiliana na changamoto hizo.

Pia aliwataka kutumia fursa hiyo ya mafunzo vizuri kwa kuwa serikali imejipanga vyema kuwainua na kuwasaidia wahitaji wote kutokana na kutenga fedha nyingi katika halmashauri, hivyo wanachotakiwa kufanya ni kujituma .

Aliongeza kuwa baada ya kupata mafunzo hayo jambo la msingi ni kuyatekeleza kwa sababu utekelezaji wao utapunguza mazingira ya vitendo vya uhalifu na ukatili wa kijinsia katika jamii zao huku akiwataka kuwatumia viongozi wao wakati wanapohitaji msaada

Wakizungumzia baada ya mafunzo hayo, baadhi ya wanufaika hao walisema wamejipanga vyema katika kuyapokea kwa kuwa wanaamini ndoto zao za muda mrefu zitatimia lakini pia wataweza kumudu maisha yao pamoja na kuzikabili changamoto za maisha kwa ujumla.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Dk. Heriel Mfangavo, alisema mafunzo hayo yamejikita katika kuwasaidia vijana namna ya kujitegemea katika nyanja zote ili kujikwamua katika changamoto wanazozipitia lakini pia kujiinua kiuchumi kwa kufanya shuguli za ujasiriamali

Dk. Mfangavo aliongeza kuwa vijana ambao wanastahili kukaa kwenye makundi baada ya mafunzo hayo, wananufaika kwa kupata mikopo kutoka katika bajeti za halmashauri ambayo itawasaidia katika kuendeleza biashara zao lakini pia vijana ambao ni wenye ulemavu wanapewa kipaumbele cha kukopeshwa au kuingizwa kwenye fursa za ajira rasmi.

# Tatizo la maji kuwa historia

**Na Happy Severine,** ITILIMA

WAKAZI 3,650 wa kijiji cha Bunamhala Mbugani, Itilima mkoani Simiyu, wanatarajia kuondokana na tatizo la maji safi na salama kutokana na kutekelezwa kwa mradi mkubwa wa maji wa Bunamhala.

Mradi huo unaotekelezwa kwa fedha za UVIKO- 19, utaongeza upatikanaji wa maji safi, salama na yenye kutosheleza kwa kiasi kikubwa na vijiji 29 vitapitiwa na mradi huo.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini ( RUWASA) wilayani Itilima, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, Meneja wa RUWASA wa wilaya, Yahya Hassan, alisema kupitia fedha za UVIKO- 19, Sh. milioni 498.5 zitatumika kukamilisha mradi huo wa Bunamhala.

Alisema wananchi wengi wa kijiji cha Bunamhala wamekuwa wakiteseka kusaka maji kwa zaidi ya miaka 30 huku wakitumia maji ya madimbwi na mito ambayo si salama kwa afya zao.

Naibu Waziri Mahundi alizipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa na Itilima kwa utekelezaji mzuri wa mradi wa uboreshaji huduma ya maji kwa ustawi wa taifa katika kupambana na maambukizi ya UVIKO - 19.

Mbali na kuwapongeza, alizitaka mamlaka zingine za maji nchini kuiga mfano huo kwa kuwatumia wataalamu wa ndani kufanya kazi nzuri.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Itilima, Faidha Ally, na mwenzake wa Maswa, Aswege Kaminyoge, waliishukuru serikali kuwaletea mradi huo mkubwa wa maji utakaokuwa mkombozi kwa wananchi ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu kusaka maji tena maji ya malambo na mabwawa ambayo si safi na salama.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MAUWASA, Mhandisi Nandi Mathias, alisoma taarifa ya mradi huo iliyobainisha kuwa Sh. 509, 884, 320 zitatumika kukamilisha mradi huo.

Alisema kazi zilizopangwa kutekelezwa kwenye mradi huo ni pamoja na uchimbaji wa mtaro na kulaza bomba na kufikia urefu wa kilomita 21.65, ujenzi wa vituo vinne vya kuchotea maji na ujenzi wa chemba 10.



## Viongozi vijiji wakumbushwa upandaji miti

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

VIONGOZI wa vijiji na kata katika wilaya ya Chemba mkoani Dodoma wametakiwa kuunga mkono juhudi za serikali za upandaji na utunzaji miti kwa kuwaelimisha wananchi kuacha kuharibu mazingira kwa kukata miti hovyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi isiyo ya Kiserikali ya Rafiki Wildlife Foundation, Clement Matwiga, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na makundi mbalimbali ya viongozi katika maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani yaliyofanyika katika Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) Pori la Akiba la Swagaswaga .

Matwiga alisema viongozi wakiungana na serikali katika jitihada za kupanda na kuitunza miti na kuwaelimisha wananchi hakutakuwa na uharibifu huo.

Alisema hivi sasa kwa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dodoma yameharibiwa kwa kukatwa miti na uchomaji mkaa.

"Asasi ya Rafiki Wildlife Foundation kwa miaka minane sasa imekuwa ikishirikiana na serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwepo kwa faida ya miti ikiwemo ya kivuli na matunda kwenye mikoa mbalimbali ikiwemo Kilimanjaro, Tanga, Singida, Simiyu, Dodoma na Manyara," alisema.

"Taasisi Mashirika na watu binafsi, ni imani yetu pia itaungana na serikali katika kuiunga mkono juhudi hizo kwa malengo ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani kwa kupanda na kuitunza miti,na kuwaelimisha wananchi kuepukana na uharibifu unaofanywa wa mazingira," alisema.

Naye Kaimu Kamanda wa Kituo cha Pori la Akiba la Swagaswaga wilayani humo, Ramadhani Abdi, aliziomba shule za msingi na sekondari kutenga maeneo ya kuotesha miche ya miti ya matunda na kivuli ili kupata mbao kwa ajili ya utengenezaji wa madawati.

Meneja Uhusiano wa Asasi ya Grument Fund, David Mwakipesile, alisema wataendelea kushirikiana na serikali na wadau wa mazingira katika uhifadhi na ulinzi wa uoto wa asili ili kuifanya Mikoa kuwa ya kijani.

# MILIONI 13 KUNUFAIKA NA MPANGO KIDIJITALI

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (DTP) unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021-2026), umepanga kufikisha huduma ya mawasiliano kwa watumiaji milioni 13 nchini.

Mradi huo wenye lengo la kukuza uchumi wa kidigitali nchini utagharimu Dola za Marekani milioni 150 na unatekelezwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Akizungumza jana kwenye kikao kazi cha kuanzisha mradi wa ujumuishwaji anuai za jamii kupitia mradi huo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema serikali imeanza kujumuisha makundi anuai ili kunufaika na mradi huo katika maeneo ya ekolojia ya kidijitali, uunganishaji wa kidijitali na jukwaa la huduma za kidijitali.

Alisema makundi hayo anuai ni pamoja na wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu, vijana na wazee.

Dk. Ndumbaro alisema lengo la mradi huo ni kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kufikia huduma za mawasiliano pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za serikali kwa wananchi kidijitali.

"Utekelezaji timilifu wa mradi wa Tanzania ya kidijitali ni pamoja na kuhakikisha ujumuishaji wa makundi anuai (jinsia, wenye ulemavu, vijana na wazee) ili kuwezesha makundi yote nchini kupata manufaa ya mradi hususani katika maeneo yote matatu ya mradi yaani ekolojia ya kidijitali, uunganishaji kidijitali na jukwaa la huduma za kidijitali," alisisitiza.

Aidha, alisema ujumuishaji wa makundi anuai utafanyika katika nyanja zote.

"Kwa kufanya hivi utekelezaji wa mradi huu sio tu utatekeleza sheria na mikataba ya kimataifa kuhusu ujumuishaji wa makundi anuai katika mipango na maendeleo ya nchi lakini pia utawezesha makundi anuai kwenda sambamba na maendeleo ya kiteknolojia yanayokwenda kwa kasi duniani,"alisema.

Kaimu Mratibu wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali, Jumanne Makumbato, alisema fedha za mradi huo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na unalenga kuboresha na kukuza maunganisho ya kidijitali ya ndani, kikanda na kimataifa.

"Kuboresha na kukuza ubunifu kwenye TEHAMA, kuimarisha na kukuza biashara mtandao, kuongeza uwekezaji kwenye sekta ya mawasiliano kwa kustawisha mazingira wezeshi kwa ajili ya matumizi na uwekezaji kwenye TEHAMA nchini,"alisema.

"Kupatikana kwa intaneti kwa bei nafuu kitaifa, kikanda na kimataifa, kuongeza weledi kwa wataalam wa TEHAMA vijana, wajasiriamali na serikali, uanzishwaji wa viwanda vidogo vya kidijitali kwa kuboresha mazingira wezeshi yanayoruhusu uwekezaji wa kisekta," aliongeza.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma, Rhobi Stephano (katikati), akipanda mti katika maadhimisho ya siku ya wanyamapori Duniani, yaliyofanyika Kimkoa kwenye hifadhi ya Pori la akiba la Swagaswaga, wilayani humo jana. Kushoto ni Kaimu Kamanda wa kituo cha Pori la akiba Swagaswaga Chemba, Ramadhani Abdi na (kulia) ni Mkurugenzi wa asasi ya Rafiki Wildlife Foundation, Clement Matwiga. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC aonya fedha za mikopo makundi maalum

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, amevitaka vikundi 18 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyopatiwa mkopo kutoka Halmashauri ya Wilaya hiyo, kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili kujikwamua kiuchumi.

Vikundi hivyo vimepatiwa zaidi ya Sh. milioni 104 na halmashauri hiyo kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Akikabidhi mikopo hiyo, Munkunda alisema: "Wanawake wengi ni waaminifu lakini wanashindwa kurudisha mikopo kutokana na kwamba akishatoka kuchukua mkopo akifika nyumbani baba anamwambia lete hiyo hela kuna dili fulani nikalipige nitapata hata milioni nane. Mwishowe anashindwa kurudisha rejesho na hela anaenda kuolea mke wa pili hiyo ndiyo changamoto kubwa."

Pia aliwahimiza kuchangamkia fursa zilizopo katika wilaya hiyo ikiwamo minada ya kila mwezi ya wilaya na kilimo cha mpunga.

Awali, akiwasilisha taarifa ya mikopo hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Denis Komba, alisema kero zilizopo ni pamoja na madeni sugu kutokana na baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo kwa wakati hasa vikundi vya vijana na watu wenye ulemavu.

Naye Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Bahi, Stewart Masima, aliwataka wajasiriamali wa vikundi hivyo kubadili fikira na kuacha kufanya biashara kwa mazoea.

Mmoja wa wanufaika wa mikopo hiyo, Deogratius John, ambaye ni mhasibu kikundi cha 'Tunaweza Walemavu' Bahi Makulu, aliishukuru serikali kwa kuwajali watu wenye uhitaji na kuahidi kufanya bidii katika kutafuta masoko.



# Wafurahia kuanzishwa wakala uwezeshaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Wanawake (UWAWAZA) umesema umefurahishwa na muswada wa kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao utasaidia na kuharakisha kupatikana kwa mikopo nafuu kwa makundi ya wanawake na kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Makamu Mwenyekiti wa UWAWAZA, Mwantatu Mbaraka Khamis, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia muswada huo.

Alisema muswada umewasilishwa kwa wakati mwafaka kuhakikisha wanawake wananufaika katika uwekezaji na kupata mikopo kwa wakati.

Alisema kwa muda mrefu kumekuwapo na mifuko mbalimbali ya wajasiriamali ambayo imekuwa ikitoa mikopo lakini bila mafanikio katika kuwakwamua wanawake kiuchumi.

Mwantatu alitaka wakala kuhakikisha kabla ya kuwapatia mikopo wanawake unaratibu mwenendo mzima wa kutoa mafunzo ambayo ndiyo yatakayoleta muongozo na kufanikiwa katika kusimamia miradi.

"Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia UWAWAZA tumefurahishwa kwa kiasi kikubwa serikali kuja na muswada wa uwezeshaji wanawake ambao sasa utasimamia mwenendo wa mikopo inayotolewa na makundi hayo na kuona wanapiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema.

Akichangia muswada huo, Mwakilishi wa Viti Maalumu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdallah, alisema mfuko huo sasa utasaidia kuratibu mwenendo mzima wa uendeshaji wa shughuli za fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi kuona zinawafikia walengwa moja kwa moja.

"Sisi wanawake tunataka kuona wakala wa uwezeshaji unakwenda kuratibu uendeshaji mzima wa fedha za mikopo za wajasiriamali ambao kwa asilimia 80 ni wanawake," alisema.

Naye Mwakilishi wa Dimani, Mwanaasha Khamis Juma, alisema muswada wa wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi sasa utayafikia makundi yote ambayo yamesahauliwa wakiwamo wanawake wa vijijini.

"Tunao wakulima wa mwani vijijini kilimo ambacho kinalimwa kwa asilimia 80 na wanawake lakini hawajafikiwa kikamilifu huku fedha hizo zikiwafikia watu ambao si walengwa," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, Sabiha Filfil Thani, alisema huu ni wakati muafaka wa kuona fedha za serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinakwenda kuratibiwa vizuri na kuwafikia walengwa.

Alisema uratibu wa fedha za uwezeshaji ni muhimu ili kuona walengwa wanapata fursa za fedha za mikopo ambayo ni kwa ajili ya kuwainuwa wananchi kiuchumi ikiwemo kundi la wanawake.

Serikali, alisema imetenga fedha nyingi kwa hivyo zinahitaji uratibu mzuri na kutungiwa sheria katika usimamizi wake ili kuona zinawafikiya walengwa kwa asilimia 100.

Akiwasilisha muswada huo mbele ya Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudriki Ramadhan Soraga, alisema kuwapo kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni hatua nyingine ya kuona wananchi wakiwamo wajasiriamali wanawake wananufaika na fursa za uwezeshaji kiuchumi.



Waziri wa Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ziara ya Samia yaongeza watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuitangaza Tanzania katika sekta ya utalii imeleta manufaa makubwa kwa kuongeza idadi kubwa ya watalii.

Hayo yalisema na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia mwelekeo wa bajeti ya Zanzibar kwa mwaka 2o22/23.

Alisema sekta ya utalii Zanzibar inazidi kupaa juu katika ramani ya utalii ulimwenguni kutokana na kazi kubwa inayochukuliwa na viongozi wakuu wa kitaifa kuitangaza kimataifa.

Lela alisema ziara ya Rais Samia aliyoifanya kwa ajili ya kutangaza sekta ya utalii imeijengea jina Zanzibar kwa kupata watalii kutoka katika kila pembe ya dunia kuanzia Asia, Ulaya Mashariki na Japan.

"Ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan imezaa matunda kwa Zanzibar kupokea idadi kubwa ya watalii ambapo mabara yote sasa yamefikiwa na watalii wake kuzuru Zanzibar," alisema.

Waziri Lela alitoa mfano wa hivi karibuni Zanzibar kupokea idadi kubwa ya watalii kutoka Ulaya kuanzia Russia hadi Ukraine ambapo watalii 900 wako Zanzibar wakiwa wamekwama kufuatia vita katika nchi yao.

Akitoa takwimu za hali ya mwenendo wa sekta ya utalii Zanzibar, Lela alisema idadi ya watalii imeongezeka na kufikia 278,754 Septemba, 2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 80 kulinganisha na watalii 154,848 katika mwaka 2021.

## Serikali kuajiri watumishi afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema mchakato wa ajira kwa sekta ya afya umeanza na kwamba utapunguza uhaba wa madaktari na wafanyakazi wa kada hiyo Zanzibar.

Mazrui alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Omar Hassan, aliyetaka kujua mpango wa serikali katika kutatua tatizo hilo kutokana na kituo cha afya kukabiliwa na upungufu wa watumishi.

Alisema wizara tayari imepokea maelekezo juu ya mchakato wa ajira kwa wafanyakazi kada ya afya wakiwamo madaktari wa Unguja na Pemba.

Waziri alisema Kituo cha Afya cha Kojani kinakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi akiwamo mtaalamu wa mashine ya kuchunguza maradhi mbalimbali (ultra sound).

Alisema ufumbuzi wa wataalamu wa kuendesha mashine hiyo utafikia mwisho wake kutokana na wizara kuanza mchakato wa ajira za wafanyakazi katika sekta ya afya wakiwamo madaktari.

Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo yamepewa kipaumbele cha kwanza katika ajira za wafanyakazi sekta ya afya ni katika vituo vya afya vilivyoko katika visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba.

"Mheshimiwa Spika nataka nimjulishe Mwakilishi wa Kojani kwamba nafahamu matatizo ya wataalamu wa kusimamia mashine ya kuchunguza maradhi mbalimbali ultra sound katika kituo cha Afya Kojani. Ufumbuzi wa tatizo hilo tunasubiri ajira za wafanyakazi wapya katika sekta ya afya," alisema.





Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MACHI 5, 2022



# HAWA WASHAMBA? Wasanii waliojipa majina ya matajiri

MJADALA umeibuka baada ya wasanii wa muziki wa hapa nchini, kujibatiza majina ya watu matajiri duniani.

Katika mitandao ya kijamii, watu wamekuwa na maoni tofauti kuhusu tabia hiyo, baadhi wakipinga na wengine wakiwatetea kwa kusema ni njia ya kujigamba.

Msanii wa kwanza kujiita jina la mtu tajiri ni Diamond Platnumz, ambaye alijiita Dangote, jina la raia wa Nigeria ambaye inasemekana ndiye mtu tajiri katika bara la Afrika.

Hivi karibuni Harmonize, naye ameibuka na kutaka kuitwa jina la mfanyabiashara na mmiliki wa klabu ya Azam, Said Salim Bakhresa.

Kama haitoshi, Rayvanny, ametambulisha wimbo wake mpya na ametaka aitwe Bill Gates tajiri na mfanyabiashara maarufu duniani.

Wanaopinga dhana ya wasanii hao kujiita majina ya watu matajiri, wamesema ni ushamba wa kisanii kwani wanaonekana kufilisika kwa kujiita majina ambayo kimsingi hawanufaiki nayo.

"Hakuna msanii anayelipwa kwa kutumia majina hayo, kimsingi wasanii wetu hawajitambui kama wenzao wan chi nyingine ambao wanatumia majina yao kama chanzo cha kipato," amesema Shaibu Juma.

Amesema wasanii wa Marekani na nchi nyingine hawana tabia ya kutumia majini ya matajiri kwa sababu wanatambua jina ni moja ya kitambulisho chake na inachangia kipato chake kama biashara nyingine.

Hata hivyo, kuna baadhi wanatetea kwa kusema kwamba hakuna tatizo kwani wasanii hao wapo katika kujigamba zaidi kwa kutokana na mafanikio wanayoyapata.

## BASI SAWA

### Pili Kitimtim unawapa kazi wenzio



MCHEKESHAJI maarufu nchini, Gladness Kifaluka, maarufu kama 'Pili Kitimtim' amewapa wakati mgumu mashabiki wake kupendekeza nani awe mume wake mtarajiwa.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Pili Kitimtim, ameeleza ana hamu ya kuwa na mume, lakini bado hajafahamu mume wake atoke mkoa gani.

Baada ya swali hilo, mashabiki wake walitiririka kumtajia mikoa ambayo anaweza kupata mume anayemfaa, huku wengine wakimtahadharisha baadhi ya maeneo.

### Mzee Mjegeje kakumbuka ya kale



MSANII wa ucheshi, Omary Abeid, maarufu kama 'Mzee wa Mjegeje' anakumbuka jinsi maisha yalivyompiga na kuamua kumuacha mke wake kipenzi.

"Nilikuwa na mke wangu bahati mbaya maisha yalikuwa magumu, nikaanguka kidogo kifedha nikasema mwanamke sio nyanya wala kitunguu umkatekate umle, ikabidi nimrudishe kwao na nikampa na talaka". Amesema

Mzee Mjegeje ameongeza kwamba mwanamke huyo alizaa nae mtoto mmoja na sasa hivi ameshaolewa na mwanaume mwingine.



# Rayvanny, Marioo wana nini kwani?

WAKALI wa muziki wa kizazi kipya, Rayvanny, na Marioo, wanataka kuwapagawisha mashabiki wao kwa kuwaletea kazi ambayo inaonekana kuwa moto mkali.

Wawili hao, wameonekana wakiwa pamoja wiki hii katika studio anayomiliki Rayvanny ya Next Level, pamoja na Prodyuza mkali S2Kizzy.

Hata hivyo, wasanii hao bado hawajasema chochote kuhusu ujio wao huo, lakini wadadisi wengi wa muziki wanasema kutokana na vipaji vya wasanii hao, ngoma hiyo itatisha.

Inavyoonekana trending ya wasanii wa Bongo kujiita majina ya wanyama huenda ikapotea baada ya baadhi yao kuelekeza nguvu zao kujiita majina ya matajiri au wafanyabiashara maarufu duniani.

# Kiapo cha Maumivu: Moyo wa uvumilivu sawa na dhahabu

**Na Adam Fungamwango**

WENYE moyo wa kuweza kuvumilia hadi mwisho ndiyo wanaofanikiwa. Ni msemo wa enzi na enzi. Hutumika kuwafanya watu wasikate tamaa licha ya magumu wanayopitia.

Pamoja na kwamba ndoa ni tukio jema la heshima, kiasi kwamba binadamu wengi kutaka kuwa nayo kwenye maisha, lakini huhitaji umakini, ujasiri, uimara wa kiakili na uvumilivu.

Kuna watu wanapenda ndoa kwa sababu tu ya hafla tu au sherehe zinazofanyika pale. Wengine tamaa tu za kimwili. Ukweli ndoa ni zaidi ya hivyo. Kuna wakati ukiwa ndani unaweza kujuta na kudhani ndiyo kitu kibaya zaidi duniani kuwepo. Lakini ukivumilia hadi mwisho na kuyashinda majaribu yote, ndiyo utaona utamu na raha ya ndoa.

Tuiangalie ndoa kwenye filamu ya 'Kiapo cha Uvumilivu'. Imechezwa na wasanii Nassor Bakari, Angel Mjema, Amly Amily, Margareth Emmanuel, Sutlan Mohamed, Michael William, na wengineo.

Chobi na mkewe Karata wameoana kwa lengo la kufurahia ndoa yao hadi mwisho wa maisha yao. Baada ya mwaka mmoja hali ikaanza kugeuka. Ni baada ya Karata kupata ujauzito mara tatu, lakini zote zinatoka kwa namna ya kushangaza.

Kutopata mtoto kunamfanya mama Chobi na binti yake kuanza kumsakama Karata na kumpa kila aina ya majina mabaya. Mwanzoni Karata alipata ulinzi kutoka kwa mumewe Chobi hata hivyo kadri siku zilivyozidi kusonga mbele, mume naye alichoka kumtetea mkewe. Naye akawa anataka mtoto.

Mke ananyanyaswa, akawa kama hausigeli badala ya mke. Ni matusi, kejeli na dharau. Akaenda kwa wazazi wake kushtaki. Wazazi wakamwambia aje na mumewe. Chobi akakataa kwenda na kuzidi kumtesa mkewe.

Rafiki yake mmoja alimshauri Chobi aende kwa mpiga ramli labda kuna namna.



Na kweli, mpiga ramli akamwambia kuwa mama yake mzazi ndiye anayefanya yote haya kwa sababu amejiingiza kwenye chama cha wachawi.

Lakini vile vile hata upande wa mwanamke pia kuna tatizo, ndiyo maana mke anapata ujauzito, lakini unatoka muda si mrefu.

Aliporudi alimwambia mkewe sasa amekubali kwenda ukweni kuwasikiliza. Alipofika aliomba msamaha kwa yote aliyoyafanya na kudai amegundua kuna tatizo.

Chobi pia akaenda kwa mama yake mzazi na kumweleza ukweli kuwa amegundua kuwa naye anahusika, kwani alimfunga mkewe ili asizae kwa sababu za kishirikina, hivyo amfungue na kuachana na mambo ya uchawi.

Familia zote mbili zinaweka mambo sawa na Karata sasa anapata ujauzito wa nne, ambao anajifungua mtoto wa kike, amani, utulivu, na furaha ya ndoa inarejea kama zamani.



# Kiba, Shilole hakuna kama wao

KITENDO cha mwanamuziki wa Bongo Fleva, Alikiba, kumpandisha Shilole jukwaani na kusahau tofauti zao zimepongezwa na watu wengi.

Alikiba alikubali kumkaribisha Shilole jukwaani na kuimba na kucheza pamoja huku wakishangiliwa na watu waliohudhuria tamasha hilo.

"Alikiba umefanya kitu cha kutisha hasa kwa wasanii wetu wa muziki, suala la kusameheana ni tukio kubwa na linatakiwa kuigwa na wengine," amesema shabiki mmoja.

## NGOMA TAMU ZA FEBRUARI

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI wa mapenzi umemalizika. Februari ni mwezi ambao wengi wameubatiza kuwa ni wa mapenzi, kutokana na kuwepo kwa siku ya 'Valentine Day'.


Hii ni sikukuu ya wapendanao ambayo huadhimishwa duniani kote Februari 14 ya kila mwaka, ingawa si siku rasmi inayotambuliwa kimataifa.

Hakuna nchi ambayo inasimamisha shughuli zake za uzalishaji kutokana na siku hii kama sikukuu zingine za kidini na kiserikali, ila wananchi wenyewe, kila mmoja na mtu anayempenda, au familia husherehekea wenyewe, nyumbani au sehemu yoyote ile ya kijamii ambayo wataona inafaa kufurahi pamoja.

Hapa nchini wasanii wengi wametoa ngoma zao kwenye mwezi huo, ambao tayari tumeuacha.

Ni ngoma zilizowachengua mashabiki wengi na kupendwa sana kwenye mwezi huo wa wapendanao.

**Gidi-Diamond Platnumz**




Ni mwezi ambao hata msanii bora kabisa kwa sasa si Tanzania tu, bali Afrika nzima kwa sasa, Diamond Platnumz ametoa ngoma yake mpya. Inaitwa 'Gidi'.

Kama kawaida, mkubwa ni mkubwa tu. Ngoma hiyo imeachiwa Februari 19 mwaka huu. Na hadi wiki hii inamalizika ilikuwa imetazamwa na watu milioni 3, 283, 316 kwenye mtandao wa You tube.

**Toroka-Anjela ft Harmonize**

Ingekuwa mwezi haujamalizika kama Diamond Platnumz katoa ngoma, halafu Harmonize akae kimya, kama siyo wimbo wake, basi hata wa kushirikishwa. Watu wangeongea nini kwenye mitandao ya kijamii?

Wangebishana nini? Harmonize hakuwa nyuma, kwani ameshirikishwa na msanii Anjela kwenye ngoma ya 'Toroka'. Hii nayo imetoka Februari 19, na mpaka mwishoni mwa wiki hii, kwenye mtandao wa Youtube wa Anjela, watazamaji milioni 1, 860,428, walikuwa tayari wameshaitazama ngoma hiyo.

**Mwambieni-Zuchu**

Msanii wa kike anayeendelea kutamba kwa sasa nchini, Zuchu, mapema kabisa, Februari 4, alitoka na ngoma, akaiita 'Mwambieni', ambayo imetikisa mno kwa mwezi huo, hasa kipindi cha kuelekea 'Valentine Day'.

"Mwambieni mali yake imeshaliwa, jimbo limeshachukuliwa, ameacha kopa, amelamba galasa…" ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye pini hiyo.


**Only You-Macvoice ft Mbosso**

"Nina nini sijui? Umenipa nini kitamu, hakipandi chakula hadi unilishe, usingizi sipati hadi wewe ulale.." Siyo maneno yangu. Hayo yamo kwenye wimbo uitwao 'Only You'. Huu ni wa msanii Macvoice akimshirikisha msanii Mbosso.

Ngoma hii imetoka siku mbili kabla ya 'Valentine Day', Februari 12.

**Yanga Tamu-Marioo**

Ilikuwa ni Februari 21, wakati msanii Marioo, alipotoa ngoma ya 'Yanga Tamu'. Ni wimbo ambao ameimba kwa kuisifu klabu ya mpira wa miguu ya Yanga.



## Kemi utamuuaje mwenzio yu hai?

UTATA umeibuka baada ya nyota wa mitandao nchini Nigeria, Kemi Olunloyo, kutoa salamu ya rambirambi ya kifo kwa mshiriki wa zamani wa Big Brother Nigeria, Tacha.

Ujumbe huo ambao umewashtua watu wengi, uliandikwa kimakosa na Olunloyo, katika ukurasa wake wa Twitter, ukisema "Ulale mahali pema peponi" wakati Tacha yupo hai.

Baada ya ujumbe huo, mashabiki wa Tacha walivamia ukurasa wake wakitaka kujua ukweli jambo ambalo lilikanushwa baadae.



## Young Thang kama kweli wafuate Ukraine

NYOTA wa muziki wa kurapu kutoka Nigeria, Young Thug ametoa ofa ya kuwatoa wanafunzi wa kiafrika walioko Ukraine, huku akifungua milango ya kuwakaribisha kujiunga kwenye chuo chake.

Hatua hiyo inatokana na usalama katika nchi hiyo kuwa mbaya kutokana na mashambulizi ya mabomu yanayoendelea kila siku kutoka kwa Russia.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram nyota huyo aliandika kwamba kama kuna vijana wa kiafrika ambao wapo ndani ya nchi hiyo hadi sasa yuko tayari kuwatoa nje ya mipaka ya nchi hiyo.

## Timaya ukinusurika utakuwa makini

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Timaya ametiwa mbaroni baada ya kutuhumiwa kufanya mauaji ya msichana mmoja.

Kulingana na taarifa iliyotolewa katika ukurasa wa Instagram wa Osinubi Omowumi, ambaye awali alilalamika dada yake kufariki kutokana na majeraha aliyopata katika tukio la kugongwa na gari.

Msanii huyo alikamatwa na polisi Jumanne asubuhi kwa ajili ya kwenda kuhojiwa kutokana na ajali hiyo anayodaiwa kusababisha na hatimaye msichana huyo amepoteza maisha.





## Julia penzi la Kanye limekuchanganya

MWIGIZAJI nyota wa Marekani, Julia Fox, amesema katika muda wa wiki sita ya uhusiano wake wa kimapenzi na rapa Kanye West, umemfanya kuwa na furaha zaidi.

Mrembo huyo kutoka Hollywood, amekiambia kipindi cha runinga cha burudani, kuwa hakuna jambo zuri katika maisha yake kama kuwa na mwanamuziki huyo.

"Ilikuwa ni kitu kizuri kukipata kwangu, ni jambo la kipekee ambalo linanirudisha nyuma kwenye maisha yangu ya kutosahau kuhusu hilo," amesema.


## Kim kawa Singo, vidume mnatakiwa

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha runinga kinachohusu maisha, Kim Kardashian, hatimaye ametangaza kuwa hayupo rasmi katika ndoa na aliyekuwa mume wake KanyeWest.

Kim ambaye ni mama wa watoto wanne, amesema hayo akiwa Los Angeles, mbele ya Jaji wa Mahakama ya Juu Steve Cochran, wakati alipowasilisha ombi la kusikilizwa haraka kesi yake ya talaka.

Akiwa mahakamani hapo, Kim amejibu ndiyo pale alipoulizwa na jaji kuwa yupo tayari kubadilisha jina lake na ndoa hiyo kuvunjwa.

Baada ya maswali hayo, jaji huyo alimwambia yupo huru na amevunja rasmi ndoa yake na Kanye West.



# Siku saba za mateso na damu alizotumia msichana wa Tanzania kujiokoa Ukraine

**Mwandishi Wetu**

VITA vinavyoendelea nchini Ukraine, imekuwa mahangaiko makubwa kwa watu wanaoishi miji mbalimbali, lakini kwa wanafunzi wa Kiafrika wamejikuta katikati ya hofu na mashaka kuhusu vipi wanaweza kujiokoa katikati ya mapigano hayo.

Hata hivyo mwanafunzi huyu wa kike kutoka Tanzania, amejikuta akitumia ujasiri wa hali ya juu kujiokoa ikiwamo kutembea kwa miguu kilomita 20 .

Nenyorata Teveli (23) ameishi nchini Ukraine kwa takriban miaka minne akisomea udaktari tangu mwaka 2017 akiwa na miaka 18 pekee.

Miaka yote aliyoishi nchini humo hali ilikuwa shwari na hakutarajia siku moja mambo yatakuwa mabaya na kukatisha ndoto zake za kuwa Daktari.

Mzozo uliokuwa ukifukuta kati ya Urusi na Ukraine, uliibua vita kamili na hapo ndipo Nenyorata , alipojikuta yupo katikati ya milio ya risasi na mabomu kutoka ndege za Russia.

Kama ilivyo kwa wanafunzi wengine muda wa kupumzika wanakwenda hosteli , Teveli na yeye alikuwa chumbani kwake amelala, lakini alikatishwa ghafla usingizi wake na mlio mkubwa wenye kishindo.

Harakaharaka hakujua ni nini, alipochungulia nje aliona moshi na moto ukiwaka katika moja ya maeneo jirani na alikokuwa anaishi. Ilikuwa siku ya kwanza ya mashambulizi ya Russia nchini Ukraine, Februari 24 mwaka huu.

Anasema milio hiyo yenye kishindo yalikuwa ni mabomu yaliyopigwa kwa takribani dakika 15 mfululizo. Akiwa mtanzania pekee katika makazi alipokua anaishi na wanafunzi wenzake, wote hawakujua cha kufanya muda huo.

Akalazimika kutoka kitandani kujua nini kinaendelea, Nenyorata aliona wanafunzi wenzie raia wa Ukraine wakibeba mabegi na kukimbia, wanasema wanaenda kutafuta hifadhi katika miji ya jirani kwani mji wao Kharkiv unashambuliwa na mabomu.

Anasema tahadhari zilianza kutolewa na watu wote kuambiwa watafute hifadhi katika mahandaki. Kwa mujibu wa Nenyorata nyumba nyingi nchini Ukraine zina mahandaki na hata baadhi ya hosteli zilikua na mahandaki lakini bahati mbaya katika hosteli yao hakukuwa na handaki.

Kwa haraka ilimbidi awapigie watanzania wenzie kwa njia ya simu kwa ajili ya kupata msaada, walikubaliana kukimbilia kwenye kituo cha karibu cha treni cha chini ya ardhi.

Akiwa na hofu ya hali ya juu, alianza kutembea akiambatana na Watanzania wengine waliokutana wakiwa hawajui nini kinaendelea.

Katika msafara huo, walikuwepo na watu wengine kutoka mataifa mbalimbali ambao nao walikuwa na nyuso zilizojaa woga, wakitumaini pengine kesho yake hali itarudi kama zamani.

**VURUMAI KUTOA PESA ATM**

Wakiwa njiani kwenda kwenye kituo cha treni kujificha kukwepa mabomu , njiani waliona watu wakikimbilia kwenye maduka kununua vyakula na misururu mirefu ya watu katika mashine za ATM wakitoa pesa.

Na yeye aliona vyema atoe akiba yake ya fedha imsaidie mbele ya safari, akatumia saa mbili kuifikia mashine ya ATM aliyohitaji kuitumia, lakini hakufanikiwa kupata pesa kwani ziliisha.

Muda ulizidi kwenda mpaka kufika kwenye kituo cha treni. Alipofika akili yake ilikuwa ni kupata pesa, bila hivyo asingejua namna gani angeishi. Jioni akalazimika kutoka tena kwenda kwenye ATM na kupata kiwango kidogo cha pesa kama Dola 100 sawa na shilingi za kitanzania kama laki mbili.

Baada ya kupata kiasi hicho cha pesa, alitumia ujasiri wa kutoka kwenda mitaa ya jirani kununua maji na vyakula vikavu ambavyo haviwezi kuharibika haraka na kisha alirudi haraka kwenye handaki.

Ndani ya handaki ambalo ni kituo cha treni, Nenyorata alikaa siku mbili bila kuwa na matumaini ya kupata msaada wa kuokolewa.

Baada ya kuona hali inazidi kuwa ngumu, aliwapigia wazazi wake kwa ajili ya ushauri na hapo alipata mbinu nyingine angalau inaweza kumpatia mwanga.

Alijaribu kuwakusanya watanzania wenzake ambao wapo ndani ya handaki na kupanga kutorokea mji wa Kharkiv, kuelekea mji wa Lviv ambao uko karibu na mpaka wa nchi ya Poland.


Wote walikubaliana kuondoka, lakini tatizo likawa wote wana hofu ya kufika huko na hatimaye kuwa na matumaini ya kurudi Tanzania.

**SAFARI YAANZA KWA TAHADHARI**

Haikuwa rahisi kutoka hapo kwa kutumia treni kutokana na kuwepo na msongamano wa watu kutoka mataifa mengine, hivyo kuingia kwenye usafiri wa treni ilikuwa ni kwa kugombea.

Hata hivyo, upande wake alifanikiwa kuingia ndani ya treni baada ya kulazimika kuacha mizigo yake.

Hata hivyo, simanzi ilimjaa pale alipowaona watanzania wenzake na raia wengine wamebaki chini baada ya treni hiyo kujaa.



NENYORATA TEVELI

Treni ilitembea kwa siku nzima, huku Teveli akiwa ni miongoni mwa watu wengi waliosimama hadi mji wa Lviv.

Licha ya kubanwa na haja, ilikuwa ngumu kwenda chooni kutokana na mrundikano wa watu. Anasema kwa saa 24 ndani ya treni hakuweza kwenda chooni, hapakuwa na pakukanyaga, kutokana na watu kubanana.

Waliwasili Lviv majira ya saa kumi na moja jioni, siku iliyofuata wakiwa hoi wamechoka lakini wakishukuru walau wamefika mji wa Ukraine ambao haujapigwa mabomu.

Baridi lilikuwa kali kiasi cha barafu kuendelea kuanguka. Teveli hakujali hali hiyo, ilikuwa ni faraja kwake kujiona yuko salama.

Angalau muda huo waliweza kupata chakula. Huku mamlaka zikichukua taarifa za kila mmoja waliofika kwenye eneo hilo la kituo cha treni katika mji wa Lviv.

Usiku ulipoingia zaidi, walilazimika kulala uwanjani, kwenye uwanja wa mpira wa kikapu. Wakitumia matandiko duni waliyopewa na mamlaka.

Siku iliyofuata waliamka mapema na kuanza safari kuelekea kwenye mpaka wa Ukraine na Poland.

Ilikua ni majira ya saa tano na nusu asubuhi waliingia kwenye gari kutoka Lviv kuelekea katika mpaka wa Poland katika eneo linaloitwa Krakovets.

Kufika mji wa Krakovets ilikuwa ni kilomita 50, lakini gari walilopanda liliwasogeza kilomita 20 tu.

Foleni ilikuwa ndefu kufika mpakani, gari za abiria zilikuwa zimejaa kupita kiasi.

Nenyorata na watanzania wenzake takriban ishirini walilazimika kutembea kwa mguu. Walitembea kwa takriban saa moja lakini bado walikuwa wanahitai kutembea kilomita 26 kufika katika kituo cha mpaka huo. Wakazi vijiji vya jirani waliwapa lifti kuwasogeza kijiji kinachofuata walipo washusha waligeuza kurudi vijijini kwao. Ulikuwa ni msaada mkubwa kwao kwani walipata kupumzika kwa dakika chache kabla ya kuanza kutembea tena.

Walitembea mpaka walipopata lifti nyingine wakafika kwenye kituo kimoja ambapo wanakijiji walikuwa wameandaa chakula na maji kwa ajili ya watu ambao hawana chakula na wanapita kuelekea mpakani.

"Kila mwanakijiji ameleta chakula hapo, hawa ni watu ambao nchi yao ipo vitani hawajui kesho itakuwaje ila walitujali na kutupa chakula chao bure" anasema Teveli.

Baada ya hapo Nenyorata na wenzake waliendelea kutembea kwa mguu ili kuufikia mpaka.

Giza linaingia, lakini wanaona mwanga wa magari na taa kwa mbali, lakini hawajui wamebakiza kilomita ngapi kufika mpakani. Muda huo walikuwa wametembea kwa mguu kwa takriban masaa sita 6. Walipokuwa katika kijiji kimoja, waliambiwa zimebaki kilomita tatu tu, ila wanatembea wanaona hawafiki.

Ilipofikia kiza kamili walifanikiwa kuingia katika kituo cha mpaka wa Ukraine na Poland. Hapa walihitaji kufuata taratibu za uhamiaji kwa kupata mhuri wa kutoka Ukraine, lakini iliwabidi wasubiri sana kwani magari yalipewa kipaumbele kuliko watu waliotembea kwa mguu. Walipanga foleni kwa muda mrefu sana mpaka kundi lao lilipoitwa wakapata fursa ya kugongewa muhuri na kuingia Poland.

Ilikuwaje walipowasili Poland?

Nenyorata anasema nchini Poland walipokelewa vizuri.Wanawake na watoto hawakupanga mstari. Hivyo walipanga mstari wakapigiwa tena muhuri wa kuingia Poland. Na hapo walipewa siku 53 za kukaa Poland na waliruhusu wakimbizi wote kuingia katika nchi hiyo bila viza.

Hapo walichukuliwa na kupelekwa katika kambi ya wakimbizi iliyoandaliwa jirani na mpaka na walikuta watu wa maeneo mbalimbali wakipewa malazi na chakula.

Kambi ilikuwa inatoa usafiri wa bure kwa wale wote wanaotaka kwenda katika miji mingine ya Poland.

Kwa bahati nzuri mwakilishi wa serikali ya Tanzania aliwasili mapema na kuwachukua Nenyorata na wenzie. Hapo walipelekwa kupanda treni bila kulipa pesa yoyote kwani serikali ya Poland iliidhinisha usafiri wa umma kutolewa bure kwa wakimbizi wote.

Hapo ndipo alipotengana na Watanzania wenzake ambao baadhi walienda Lublin na wengine walienda Warsaw mji mkuu wa Poland.

Nenyorata sasa anaendeleaje?

"Mimi sijambo ila ni uchovu tu, naendelea vizuri ila ningependa kuishukuru sana serikali yetu ya Tanzania kupitia ubalozi wake wa Berlin na Sweden kwa kutushika mkono," anasema Nenyorata.

Anashauri Watanzania wanaoendelea kuvuka mpaka serikali iweke utaratibu maalumu wa kuwapokea kwa kuwapa chakula na malazi.

Anasema pesa za Ukraine ziko juu kuliko za Tanzania na sio kila mzazi anaweza kumudu hizo gharama. Kuna wengine wameletwa na wafadhili na wao wanalipia ada tu. Hivyo serikali ikiweka utaratibu utasaidia kuwaokoa.

**BBC**

TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Historia ya mchezo wa karata duniani

## ●Unajua maana ya jembe, kisu, na kopa?
## ●Kwa nini kuna jike, mzungu wa nne?



Na Adam Fungamwangu

HAPA mchini Tanzania, mchezo wa karata ulikuwa ni moja ya michezo pendwa mno miaka ya nyuma ambapo ilikuwa huwezi kukatiza mitaa minne au mitano bila kukuta akinadada au akinamama wanacheza barazani.

Wakati wa mchana wakishakula na kufanya kazi zao za kawaida, basi hujiburudisha na mchezo huo. Hata wanaume nao kwa nyakati fulani wakiwa wamejipumzisha, au siku za mapumziko, wamekuwa wakicheza mchezo huo, ambao kama ukiwakuta wanacheza inakuwa ni burudani tosha, kama vile michezo mingine inavyokuwa ikiwemo bao.

Utakuta wanabishana kama vile mchezo wa soka. Wengine wamekuwa wakicheza kwa kupitisha mchana, kama hawana majukumu siku hiyo yanayowakabili.


Ulikuwa ukichezwa kwa mitindo mbalimbali, kama vile 'albastini', 'mapiku', 'last card' na mingine mingi, ili mradi tu ulikuwa ni mchezo uliokuwa ukipendwa mno na kuvuta hisia za wengi, ukichezwa kabla au baada ya chakula na watu wa familia moja, majirani au wanaoishi nyumba moja, hasa za kupanga.

Ukiacha hapa nchini, huu ni mchezo maarufu sana duniani ambao ulianza karne na karne zilizopita.

Acha wale waliocheza kwa kujiburudisha, lakini wengine walicheza kwa ajili ya kipato, yaani kamari.

Kwa sasa unaonekana ni kama umepoteza mvuto Tanzania, ingawa bado kuna watu wanaendelea kupambana kucheza.

Mabadiliko au maendeleo ya teknolojia yamesababisha mchezo huo kudorora, au kuonekana hauchezwi sana, kwa sababu hata wale wapenzi wa mchezo huo wameonekana kucheza zaidi kwenye simu zao janja, ambako kuna michezo mbalimbali, ikiwemo hata huo wa karata. Unaweza kucheza mchezo huo kwa kutumia teknolojia hiyo kwa sasa.




Historia ya mchezo huo

neno karata linatokana na jina la kireno 'Carta', ambalo kwa kilatini linamaanisha karatasi.

Historia inasema kuwa karata zilianza kutumika nchini China kwenye karne ya tisa, ingawa hawakutumia kama hizi za sasa, badala yake ni karatasi zilizochorwa kwa mkono. Baadaye walianza kutumia pesa kama karata, kitu ambacho kilikuwa hatari na kinyume cha sheria, wakarejea kwenye utaratibu wao wa awali. Ukajichukulia umaarufu sana bara la Asia, na ilipofika karne ya 11 ukafika nchini Misri.

Kwenye karata kuna maua ambayo yamekuwa yakimpa taarifa mchezaji namba ya kucheza. Maua haya ni manne, ambayo ni jembe au shupaza, moyo, maarufu kama kopa, kisu na mavi ya mbuzi kwa lugha ya Kibongo.

### Maana ya kopa, jembe na kisu

Inaelezwa kuwa nembo hizi nne za kwenye karata zilibuniwa nchini Ufaransa na mavi ya mbuzi inawakilishwa na wakulima kazi zao za mikono, moyo au kopa ni maisha ya binadamu na mapenzi, yaani furaha ya mwanadamu siku zote duniani hutokana na mapenzi, kisu inawakilisha wafanyabiashara zao na harakati zao za kuusaka utajiri, huku jembe au shupaza ni majemedari au mahodari wa vita.

### Jike, mzungu wa nne, jokeli

Kila kitu kilichomo ndani ya karata hakikuwekwa kwa bahati mbaya. Namba zote za karata zimewekwa kwa sababu maalum.

Picha zilizomo, pamoja na watu waliochorwa kwenye karata zenye nembo ya Q, J na K, wakiwa wamevaa mataji na wengine wameshika upanga, inaelezwa kuwa ni watu halisi ambao wamo kwenye historia mbalimbali za vitabu maarufu na vya kuheshimika duniani, kipindi kirefu nyuma, karne na karne zilizopita.

Nembo Q kwa hapa bongo inasomeka kama mzungu wa pili, bibi au jike, ni wanawake na malkia mbalimbali maarufu waliotajwa huko kwenye historia miaka dahari iliyopita, pia kuna mzungu wa tatu, yaani J.

Nizungumzie kwa ufupi karata ya nembo K, ambapo Bongo inajulikana kama mzungu wa nne, bwana au dume.

Ukiweka mzungu wa pili, na mwenzako akaweka dume, basi inahesabika kimchezo, aliyeweka mzungu wa pili ameolewa.

Mzungu wa nne wa jembe anaaminika kuwa ni mfalme Daudi aliyepigana vita nyingi, na wa mavi ya mbuzi anadaiwa kuwa ni Alexander, mfalme wa Masedonia, wa kwenye kopa ni Carloman, mfalme zamani wa Ufaransa, na kumekuwa na ubishi wa yule wa kwenye dume ya kisu, wengine wakidai ni mfalme wa Kirumi Kaisari Agusto, wengine wakisema ni Julius Kaisari.

Karata ya jokeli ilianza kutumika nchini Ujerumani kuanzia mwaka 1860, ambapo kulikuwa na aina moja ya mchezo iliyohitaji karata moja inayotisha. Mchoro wa jokeli ikawa pendekezo na mpaka leo hii inatumika kwenye aina nyingine za michezo hiyo.

### Dume la Shupaza

Dume la shupaza au jembe ni karata yenye upekee mkubwa kuliko zote. Kimuonekano na jinsi ilivyochorwa kwa nakshi na mikogo, ikiwa na nembo kubwa na maandishi na michoro ambayo imekuwa ikishangaza na kuvutia wengine.

Hapa Bongo ilipachikwa majina mbalimbali 'kubwa la madume', 'Robert Mandevu' na mengine mengi, huku likipewa heshima ya pekee na hadhi kwenye mchezo huo. Mtu akilamba dume hilo, kama ukiwa makini utajua tu, kwa sababu hata sura inabadilika kwa tabasamu.

Lakini si wengi wanaojua sababu yake. Katika karne ya 16 kulikuwa na kodi ya kutengeneza karata hizo huko Ulaya. Kabla hazijapelekwa sokoni, mamlaka zilitakiwa kupiga mihuri karata zote ili kuonekana kuwa zimelipiwa. Karata ya dume za shupaza ilikuwa ndiyo chaguo la mamlaka hizo kwa ajili ya kupita mhuri kwa kila nakala ili kuonekana zimelipiwa.

Wajanja walikuwepo tangu wakati huo, wakawa wanatengeza mihuri 'feki' na kugonga ili kukwepa kodi.

Mamlaka zilivyoshutuka, zikaamua kutengeneza zenyewe dume la shupaza, kugonga au kuchapisha mhuri na kuwapa watengenezaji ili wachanganye na karata zao zingine zilizobaki walizotengeneza wao. Hapo ikafahamika kama 'karata ya kunyongea', kwani ikawa kufoji mhuri wa mamlaka na kuugonga kwenye karata, iliweza kusababisha adhabu ya kunyongwa. Ndipo walipowaweza.

Na hata sheria hiyo ilipoondoka barani humo, na utaratibu huo kupita, viwanda vya kutengeneza karata havikubadilisha aina au muonekano kuwa dume la shupaza, kwa sababu ilikuwa imezoeleka machoni mwa watumiaji na waliipenda sana iendelee kubaki hivyo, kwa hiyo ikaachwa hivyo hivyo, huku kila nchi au watengenezaji wakiongeza nakshi, mbwembwe na urembo wanaoona unafaa kwenye karata hiyo dume la shupaza au 'Robert Mandevu'.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Russia yaendelea kuiangamiza Ukraine

## ●Kituo cha nyuklia chalipuliwa, meli yazamishwa baharini

RAIS wa Russia Vladimir Putin ametoa onyo kwa nchi zinazopinga hatua ya nchi yake kuingia vitani na Ukraine, kutozidisha tatizo kuwa baya zaidi kwa kuweka vikwazo zaidi.

Putin alikuwa akizungumza katika mkutano wa serikali uliotangazwa kwenye kituo cha habari cha Rossiya 24, kinachomilikiwa na serikali.

"Hatuna nia mbaya dhidi ya majirani zetu," alisema Putin.

Serikali yake haioni haja kwa majirani zake kuchukua hatua zaidi ambazo zitafanya uhusiano wao kuwa mbaya zaidi.

"Nadhani kila mtu lazima afikirie jinsi ya kurekebisha uhusiano, kushirikiana kawaida na kukuza uhusiano kama kawaida," aliongeza.

Haya yanajiri wakati mawaziri wa mambo ya nje kutoka nchi za Magharibi wakikutana mjini Brussels, Ubeligiji kutafakari jinsi ya kuishinikiza nchi hiyo kusitisha vita.

Putin pia anarudia madai yake ya awali kwamba hatua zote zilizochukuliwa na jeshi lake hadi sasa zimefanywa katika kukabiliana na baadhi ya hatua zisizo za kirafiki dhidi ya Russia.

### KITUO CHA NYUKLIA CHALIPULIWA

MAJESHI ya Russia yamekidhibiti kituo cha nishati cha nyuklia nchini Ukraine baada ya kukishambulia kwa makombora jana.

Moto ulizuka katika kituo hicho cha Zaporizhzhia ambacho ni kikubwa zaidi katika bara la Ulaya.

Hata hivyo, Ukraine ilisema kuwa kituo kilishambuliwa na wanajeshi wa Russia.

Mamlaka ilieleza kituo hicho sasa kiko salama na viwango vya mionzi ni vya kawaida.

Viongozi mbalimbali duniani wameishutumu Russia kwa kuhatarisha usalama wa bara zima, huku Rais wa Ukraine, akiishutumu kwa ugaidi wa kinyuklia.

Rais wa Marekani Joe Biden, aliitaka Russia kusitisha shughuli zake za kijeshi katika eneo hilo, huku Waziri Mkuu wa Canada Justin Trudeau, akiyaelezea kuwa ni mashambulizi ya kutisha na kusema lazima yasitishwe mara moja.

Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, alisema shambulio hilo ni la kizembe na linaweza kuhatarisha moja kwa moja usalama wa Ulaya yote.

Viongozi wote watatu walizungumza na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky kwa njia ya simu.

Wakati huo huo, Rais Zelensky, alisema Russia inataka kurudiwa kwa Chernobyl, eneo lililo shuhudia maafa mabaya zaidi ya nyuklia duniani mwaka 1986.

"Ikiwa kuna mlipuko, ni mwisho wa kila kitu mwisho wa Ulaya," alisema

Video kutoka katika kiwanda cha nyuklia ilionyesha milipuko angani nyakati za usiku na kutoa moshi mwingi.

Museveni akutana na balozi wa Russia

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, juzi alikutana na balozi wa Russia Vladlen Semivolos, kujadili masuala yenye maslahi kwa pande zote mbili.

Hakutoa maelezo zaidi, lakini ilikuja siku moja baada ya Uganda kujizuia kupiga kura kwa azimio la Umoja wa Mataifa la kulaani uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Nchi nyingine 16 za Afrika zikiwemo Afrika Kusini, Angola, Algeria na Mali hazikupiga kura.

Mtoto wa kiume wa Rais Museveni, Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba, Jumatatu alieleza kuunga mkono uvamizi wa Russia nchini Ukraine katika ujumbe wa Twitter.

### WANIGERIA KUTOKA UKRAINE WAWASILI

Kundi la kwanza la raia wa Nigeria, walioondolewa kwenye mzozo wa Ukraine wamewasili mji mkuu, Abuja majira ya asubuhi jana.

Kundi hilo lina wanafunzi 451 kwa mujibu wa mwenyekiti wa kamati ya bunge la nchi hiyo wa masuala ya kigeni, Yusuf Buba, ambaye aliandamana nao kutoka mji mkuu wa Romania, Bucharest.

Nigeria inatarajiwa kuwahamisha raia 5,000 wanaokimbia vita nchini Ukraine.

Wengi wamevuka hadi nchi jirani ya Romania, Poland na Hungary.

Zoezi la kuwarejesha kwao likusudiwa kuanza Jumatano, lakini lilicheleweshwa kwa sababu ya changamoto za usafirishaji.

Tume ya Wanigeria waliopo nje ilituma picha za kuwasili kwa wanafunzi hao katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Nnandi Azikwe.



Miale ya moto kutoka katika mtambo wa nishati ya Nyuklia nchini Ukraine baada ya kituo hicho kulipuliwa na mabomu ya Russia jana**: PICHA BBC**

### VIFO MASHAMBULIZI YA ANGA VYAONGEZEKA

Watu 47 wameuawa katika mashambulizi ya anga ya Russia yaliyolenga makazi ya watu katika mji wa Chernihiv, mamlaka ya kikanda imesema. Kazi ya uokoaji ilibidi kusitishwa siku kwa sababu ya kuwepo milipuko ya mizinga mikubwa.

Jumla ya watu 148, wengi wao wakiwa raia, wamefariki tangu kuanza kwa mapigano katika eneo hilo.

Jiji hilo lina watu 300,000 liko kaskazini mwa nchi hiyo, karibu na mipaka ya Russia na Belarusi.

Meli yazama baada ya mlipuko

Wamiliki wa meli ya mizigo kutoka Estonia, wamesema chombo hicho kimezama katika pwani ya Ukraine, baada ya kutokea mlipuko.

Walisema wafanyakazi wawili walipatikana baada ya kujiokoa katika viokozi baharini na wengine wanne walionekana baadae na wote sita walichukuliwa na huduma ya uokoaji ya Ukraine.

Meli hiyo yenye bendera ya Panama, inamilikiwa na kampuni ya Vista Shipping Agency yenye makao yake huko Estonia. Jimbo la Baltic Estonia ni mwanachama wa Nato na ina mpaka na Russia.

Meli hiyo ilikuwa imetia nanga katika pwani ya Ukraine baada ya kuondoka katika bandari ya kusini ya Chornomorsk karibu na Odesa siku kadhaa zilizopita.

Jeshi la Ukraine linasema kuwa Russia inatuma meli za kivita ili kuukamata mji wa Odesa, ambao una watu milioni moja na bandari kuu.

### MAREKANI YAWEKA TAHADHARI TIMU YA NYUKLIA

Marekani itaweka katika tahadhari kikosi cha nyuklia (NEST). Uamuzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Jennifer Granholm baada ya mazungumzo ya dharura na Ukraine.

NEST kikundi cha wanasayansi, mafundi na wahandisi ambao kazi yao ni kujibu haraka iwezekanavyo aina yoyote ya tishio la nyuklia kokote duniani.

"Operesheni ya jeshi la Urusi katika eneo la nyuklia ni uzembe kabisa na lazima usitishwe ," alisema, na kuongeza kuwa mitambo ya nyuklia imelindwa na mifumo imara na inafungwa kwa usalama.

" Hatuoni viwango vya hali ya juu vya mionzi ya nyuklia karibu na eneo ," Granholm alisema.

### RAIS WA UKRAINE AOMBA MAZUNGUMZO NA PUTIN

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amesema njia ya kumaliza vita nchini mwake ni kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na mwenzake Vladimir Putin.

"Hatutaki kuishambulia Russia na hatupangi kushambulia. Mnataka nini kutoka kwetu? tokeni kwenye ardhi yetu, "alisema Rais Zelensky.

Aliongeza kuwa, kuna umuhimu wa kufanya mazungumzo yaliyoanza mwezi uliopita.

"Njooni tuketi pamoja. Msiketi umbali wa mita 30, kama mlivyofanya wakati Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron alipokutana na Putin." Alisisitiza.

**HABARI: BBC**




Eneo la makazi ya watu na magari yakiwa yameteketezwa na makombora yanayorushwa na vikosi vya Russia katika mji mkuu wa Kyiv nchini Ukraine. **PICHA: BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KADI YA GARI

ALLI SELEMANI LAILALA ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI(TOYOTA) yenye namba za usajili T 759 BLU Chassis namba: KEFKE800001435 Injini namba : 111335907 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/81956/2022

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu ABDALLAH MOHAMED JONGO anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SUPER POWER yenye namba za usajili MC 616 AEL. Yenye Chassis No: LJEPCJL08CA006287 Na. Engine No: CYA80022 Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: TAN/RB/396360/2022

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 36 OF 2022
In the matter of the Estate of the Late JACKSON STANLEY TOLOGA of Ipagala ward within Dodoma City Council
AND
In the matter of an application for Letters of administration by AGNESS KODI TOLLOGA**

**GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22nd Day of March, 2022.
Dated at Dodoma this 02nd day of March 2022

A.K. Tolloga
..................
PETITIONER

Presented for filling this 02 day of March 2022

..................
RESIDENT MAGISTRATE

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA
SHAURI NO.53/2020
WILFRED JULIUS KASAMBALA..................MDAI
DHIDI YA
JOYCE EZEKIEL KASHILILIKA.........................MDAIWA
NMB BANK PLC................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI
KWA;
ARON MWAISA MWAKYUSA,**

Fahamu ya kwamba WILFRED JULIUS KASAMBALA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 09/03/2022 saa 2.30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
KUMBUKA;Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri /muhuri wa baraza hili leo tarehe 22/02/2022.

**T.Munzerere
MWENYEKITI
22/02/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU
WILAYA YA GEITA
SHAURI LA MADAI NAMBARI 37/2022
MDAI: SHABANI ATHANAS LUBIMBI
DHIDI YA
MDAIWA FAH CONSTRUCTION CO LTD SLP 11580 DSM@HAMIS
SALUM MPINDA WA
TANZANIA BARA NA VISIWANIPOPOTE ALIPO BARA NA VISIWANI**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 15/03/2022 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.
Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo 28 tarehe 02 Mwezi 2022

HAKIMU
..................................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA CHETI



MAYASA S. MOHAMED anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye INDEX NO. S 0432-0018 kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia shule ya JABAL HIRA MUSLIM JUNIOR SEMINARY mwaka 2015)/ P0332-0092 (morogoro secondary center mwaka 2016) yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0674942105.
POLISI TAARIFA: MOR /MOR/RB/84237/2022

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA**

**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI [SURA 334]
KUPOTEA KWA BARUA YA
TOLEO [LETTER OF OFFER] YA KUMILIKI ARDHI.**

**Barua ya toleo [ letter of offer] ya kiwanja Na.313 kitalu 'N' Kiseke.
Mmiliki aliyeandikishwa: SALVATORY RUPIA wa S.L.P 661, MWANZA.
Ardhi: kiwanja Na.313 Kitalu 'N' Kiseke, manispaa ya ilemela.
Mwombaji: MATHIAS BUBERWA RUPIA wa S.L.P 661, MWANZA**

**TAARIFA IMETOLEWA** kwamba, barua ya toleo [letter of offer] ya kumiliki Ardhi iliyotajwahapo juu imepotea na tunakusudia kutoa Barua ya toleo [letter of offer] mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi chochote kwa muda siku thelathini [30] kuanzia tarehe ya taarifa hii.
Barua ya toleo [ letter of offer] ya asili ikionekana irudishwe kwenye ofisi ya mkurugenzi wa manispaa ya ilemela S.L.P 735 Mwanza.

D.S.Tongora
KNY: MKUU WA IDARA YA MIPANGO MIJI.
MANISPAA YA ILEMELA.

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA**

**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI [SURA 334]
KUPOTEA KWA BARUA YA
TOLEO [LETTER OF OFFER] YA KUMILIKI ARDHI.**

**Barua ya toleo [ letter of offer] ya kiwanja Na.23 kitalu 'N' Kiseke.
Mmiliki aliyeandikishwa: SALVATORY RUPIA wa S.L.P 661, MWANZA.
Mwombaji: MATHIAS BUBERWA RUPIA wa S.L.P 661, MWANZA
Ardhi: kiwanja Na.23 Kitalu 'N' Kiseke, manispaa ya ilemela.**

**TAARIFA IMETOLEWA** kwamba, barua ya toleo [letter of offer] ya kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na tunakusudia kutoa Barua ya toleo [letter of offer] mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi chochote kwa muda siku thelathini [30] kuanzia tarehe ya taarifa hii.
Barua ya toleo [letter of offer] ya asili ikionekana irudishwe kwenye ofisi ya mkurugenzi wa manispaa ya ilemela S.L.P 735 Mwanza.

D.S.Tongora
KNY: MKUU WA IDARA YA MIPANGO MIJI.
MANISPAA YA ILEMELA.

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuatakama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee.

# Operesheni namba moja-16

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake.

Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

********************************

Ukweli ni kwamba ni kazi iliyofanywa na Jan. Wakati akimlenga askari mmoja, papo hapo na yeye akaamua kumpiga, ili asimuue askari, lakini alikuwa amechelewa sekunde moja, kwani tayari alikuwa amefyatua risasi. Hata hivyo ilimkosa askari aliyekusudiwa na Jan mwenyewe hakumlenga ipasavyo yule jamaa aliyejificha.

Ilionekana baada ya kujeruhiwa, jamaa yule aligeuka na kutaka kujua ni wapi risasi hiyo ilipigwa kutoka nyuma yake. Ndipo alipompa sura vizuri Jan, akamtandika kwenye paji la uso.

Kwa kazi aliyoifanya, aliona sasa hakuwa na sababu ya kuendelea kujificha. Alikuwa na uhakika kuwa askari watamtambua kuwa yeye ndiye aliyewataarifu na pia ndiye alikwenda kuuweka mkoba ule pale. Kosa lake moja tu ni kwamba hakuondoka sehemu hiyo ya hatari. Kitendo cha kuwasaidia na kuwaponya kuuawa, pia kungemfanya kuonekana shujaa mbele ya askari polisi.

Alitafuta njia ya kutaka kujitokeza akashindwa. Vyovyote vile ambavyo angejitokeza, angeonekana ni mmoja wao, hivyo angepata zawadi ya risasi.

Alifikiri kidogo, akapata wazo. Akaweka bastola yale mfukoni na kupachika kisu chake kiunoni. Akasimama na kutembea taratibu hadi sehemu ambayo hakukuwa na kichaka cha majani yaliyokuwa pembezoni mwa kingo za daraja la Kajima.

Akanyanyua mikono juu na kujitokeza mbele ya askari waliokuwa wamelala chini, kila mmoja akitafakari jinsi walivyovamiwa na watu wengine.

"Ni mimi Afande. Ni mimi niliyeweka mkoba wa pesa hapo kwenye daraja na mimi ndiye niliyewaita." Alijitokeza huku akiwa ameweka mikono juu.

"Nilikuwa nimejificha kwenye kichaka hiki, huku nimeua majambazi wawili, mmoja ni yule jamaa mfupi aliyewakimbia hapo, alikuwa amejificha pale na yeye alikuwa anataka kuwaua, nimempiga bastola."

Afande mmoja alimuamuru mwenzake, aende haraka kumsachi Jan kwa sababu za kiusalama. Siku zote kwenye mapambano huwa hakuna kuaminiana.

Bastola ilichukuliwa, na baada ya kusachiwa alikutwa na kisu. "Hivi vitu tutakurudishia baadaye, tutakapojidhihirisha kuwa ni raia mwema." alisema Afande aliyekuwa anamsachi Jan.

Askari wengine wawili walitumwa waongozane na Jan ili kwenda kuhakikisha anayosema ni ya kweli.

Askari wa tatu alikuwa nyuma na bastola akiwalinda wote watatu. Jan aliwaongoza hadi kwa maiti ya yule aliyewakimbia askari ambaye alimuua yeye kwa bastola.

"Huyu ndiye aliyekuwa akitaka kuwaua, mimi nilikuwa nyuma yake, nikampiga na bastoka." Aliwaambia huku askari wakishuhudia.

Aliwapeleka kwenye maiti ya pili ambayo ilipoteza uhai kwa kisu alichotumia, na dakika chache zilizopita kilichukuliwa na maafande.

"Huyu alipita hapa pamoja na mwenzake. Walikuwa wanakwenda kuchukua mkoba wa pesa, nikammaliza." Aliwataarifu.

Mpaka hapo Jan alikuwa amemaliza kuwaonyesha ni jinsi gani na yeye kwa nafasi yake amehusika kwenye tukio lile la kupambana na watekaji.

Waligeuza na kurudi chini ya daraja. "Afande yote aliyoyasema ni kweli. Ameua watu wawili ambao ni hatari, mmoja ni yule jamaa mfupi aliyetukimbia hapa. Ni raia mwema." Afande mmoja alimwambia mwenzake.

"Halo halo afande, huku juu tumefanikiwa kuwakamata watekaji, wakiwa na msichana waliyemteka. Tumefanikiwa kuwadhibiti, lakini tumepoteza Afande mmoja." Ilikuwa na redio call ikisema.

Kwa pale, hakukuwa tena na mtu yoyote aliyekamatwa zaidi ya maiti zilizokuwa zimetapakaa chini.

Aliyekuwa akionekana ndiye mkubwa wa kikosi hicho cha maafande aliamuru mmoja abebe mkoba ule wa pesa na kila mtu aongoze mbele kutoka eneo la chini ya daraja la Kajima kwa tahadhari.

Walipandisha juu. Kwa mbali waliona gari lililokuwa pembeni mwa daraja hilo, likiwa limezingirwa na askari polisi.

Walisongea taratibu. Ulikuwa ni usiku wa manane. Nchi ilikuwa kimya na tulivu. Hakuna magari yoyote yaliyokuwa yanapita wala mtu.

Wakati wanafika eneo hilo, alishuhudia kuna maiti tatu zikiwa chini. Moja ilikuwa na sare ya polisi.

"Afande Dusu, ni kwamba tumekabiliana na hawa jamaa waliokuwa wamekuja kuchukua mkoba wa pesa walikuwa wametuma vijana waende kuuchukua, wengine walibaki hapa kwa ajili ya makabidhiano ya msichana Diana waliyemteka, lakini tumewakabili, tumefanikiwa, lakini tumempoteza mwenzetu, Afande Marco."

**Nilikuwa nimejificha kwenye kichaka hiki, huku nimeua majambazi wawili, mmoja ni yule jamaa mfupi aliyewakimbia hapo, alikuwa amejificha pale na yeye alikuwa anataka kuwaua, nimempiga bastola.**

Mshtuko ulimpata Jan. Ni kama vile alikuwa analifahamu jina hilo. Anafahamu jina la askari mwenye jina hilo. Ndiyo askari kwenye majina kama hayo wako wengi, lakini huyu anayemfahamu yeye, yumo kwenye harakati hizi za kuhakikisha Diana anapatikana. Ndiyo ni Afande Marco, askari ambaye Jan anamfahamu kuwa mmoja wa wapenzi wake Diana.

Alijaribu kuangaza macho. Akisaidiwa na mwaga wa taa zilizokuwa pembeni mwa barabara ya Morogoro, maeneo ya karibuni kabisa na Magomeni Mapipa. Anamfahamu fika Afande Marco. Akakumbuka jinsi alivyokwenda kumwambia atoe pesa za kumkomboa Diana kama watekaji walivyotaka na yeye akamjibu kuwa hawezi kutoa, badala yake atajua jinsi gani anaweza kukabiliana na wahalifu hao.

Pamoja na kwamba Jan alijua mmoja wa watu tishio kwenye uhusiano wake na Diana, Afande Marco ameuawa, alihuzunishwa mno na kifo hicho kwani alikuwa kwenye harakati za kumuokoa msichana huyo. Alijua sasa mpinzani wake mkubwa atabaki kuwa Challa, ambaye kwake anamuona ni hatari zaidi kuliko alivyokuwa Afande Marco. Ni kwa sababu Challa ana pesa nyingi na anaweza kufanya lolote lile. Penye udhia penyeza rupia. Pesa ilivunja bonde na milima.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akiwa ameshiriki mbio za kilomita tano zinazodhaminiwa na Grand Malt katika mashindano ya Kilimanjaro Marathon yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro Jumapili iliyopita. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

# Watanzania walivyong'ara miaka 20 ya Kili Marathon

**Na Somoe Ng'itu,** aliyekuwa

MOSHI

MBIO za Kilimanjaro Marathon ambazo hufanyika kila mwaka katika Mji wa Moshi mkoani Kilimanjaro hapa nchini, mwaka huu zimetimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

**Kwa mara ya kwanza mbio hizo zilifanyika mwaka 2003 na zilishirikisha wanariadha zaidi ya 500 kutoka katika nchi 10, lakini mwaka huu ambapo kulikuwa na maadhimisho ya miaka 20, zaidi ya wanariadha 12,000 walijiandikisha kushiriki na wanatoka kwenye mataifa 58 duniani.**

Kutokana na umaarufu wake, kwa miaka kadhaa wanariadha kutoka Tanzania walionekana kushindwa kufurukuta dhidi ya wapinzani wao kutoka jirani, Kenya kwa kuchukua medali za dhahabu.

Lakini kutokana na maandalizi ya dhati yaliyofanyika mwaka huu, wanariadha wa Tanzania waling'ara zaidi ukilinganisha na miaka mitatu iliyopita kwa Wakenya kumaliza kwenye nafasi za juu kwenye mbio hizo ambazo zinatarajiwa kubadilishwa jina na kuwa za kimataifa kutokana na ubora wake.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa kwanza wa mbio za kilomita 42, Aloyce Simbu, katika mashindano ya Kilimanjaro Marathon yaliyofanyika Jumapili iliyopita.

### SIMBU AFANYA KWELI

Kwa upande wa wanaume, mwanariadha Mtanzania, Aloyce Simbu aliibuka mshindi katika mbio za kilomita 42 (Kilimanjaro Premium Lager Marathon) kwa kutumia saa 2:16:31.

Akizungumza na Nipashe kaka wa Aloyce, ambaye pia ni mwanariadha maarufu nchini, Alphonce Felix Simbu, alisema mdogo wake aliwahi kuwa mwanariadha miaka ya nyuma, lakini kuna wakati alikacha mchezo huo.

Simbu alisema Aloyce aliamua kuwekeza nguvu zake katika kilimo na ufugaji, lakini baada ya kuona maandalizi na zawadi za washindi zinaongezeka kila mwaka, aliamua kurejea na kuanza mazoezi kwa ajili ya kusaka medali.

"Hii ni medali yake ya kwanza kushinda, lakini ameshiriki kwa mara ya pili, tunashukuru Mungu amefanya vizuri, siri kubwa ya ushindi ni maandalizi ya muda mrefu aliyofanya," alisema Alphonce.

Aliongeza katika familia yao wanaupenda sana mchezo wa riadha na matunda yake yanaonekana pia kwa ndugu yao, Marco Joseph.

"Marco ambaye amefanya vizuri leo ( Februari 27, mwaka huu), ni mdogo wangu, tunatoka familia moja, ni mtoto wa baba yetu mdogo, " alisema mwanariadha huyo ambaye mwaka huu alikuwa kocha wa wadogo zake.

Nafasi ya pili katika mbio za kilomita 42 ilichukuliwa na Mkenya Arnold Kiptaoi aliyetumia saa 2:17:05 huku nafasi ya tatu ikienda pia kwa Mkenya, James Tallam aliyetumia saa 2:17:43 wakati Abraham Kipkosge kutoka Kenya akimaliza katika nafasi ya nne na Cosmas Kigen akimaliza kwenye nafasi ya tano, pia kutoka Kenya.

Washindi wengine kuanzia nafasi ya sita ni pamoja na Kenneth Omulo kutoka Kenya, Marco Joseph, Khamis Athumani, Paul Festo wote kutoka Tanzania na Amos Kipchirchir wa Kenya.

Shelmith Muriuki kutoka Kenya aliibuka mshindi kwa upande wa wanawake katika umbali huo kwa kutumia saa 2:41:06 huku nafasi ya pili ikienda kwa Mkenya Flavious Kwamboka, Angle John wa Tanzania alishika nafasi ya tatu huku Annika Berlin raia wa Ujerumani alimaliza wanne na tano bora ilikamilishwa na Angella Mburu kutoka Kenya.

Nafasi ya sita ilikwenda kwa Banuela Katesigwa wa Tanzania, Justina Kilumelume wa Zambia, Rose Mallya (Tanzania), Laurie Eastup kutoka Marekani na namba 10 ilishikwa na Lusia Assenga wa Tanzania.

Emmanuel Giniki aliibuka mshindi katika mbio za kilomita 21 zilizodhaminiwa na Kampuni ya Tigo na kufuatiwa na Gabriel Geay huku Inyasi Sulley alimaliza katika nafasi ya tatu wakati Kaposhi Laizer alimaliza wanne na nafasi ya tano ilienda kwa Shing'ande Ginniki wa Tanzania.

### MAJALIWA AZIPAISHA MBIO

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alianza kwa kuwashukuru wadhamini wote walioshiriki katika kufanikisha mbio hizo, watendaji pamoja na washiriki wote.

Kutokana na ubora wa mbio hizo, Majaliwa alisema umefika wakati sasa jina lake likabadilishwa na kuitwa International Kilimanjaro Marathon kutokana na kuhusiana washiriki kutoka mataifa mbalimbali huku yakiwa kwenye ubora wa juu.

Alisema serikali itaendelea kuwaunga mkono waandaaji wa mbio hizo pia aliwapongeza washindi wote na kuwaambia mafanikio yao yametokana na jitihada walizozifanya.

Naye Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, alimpongeza Waziri Majaliwa kwa kuonyesha mfano wa kushiriki mbio za kilomita tano.

Gekul alisema pia wanaishukuru serikali kwa kutengua kiasi cha Sh. Bilioni 1.5 na kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), wizara itazitumia katika kukuza vipaji huku akiahidi shule za michezo 56 zinazojengwa zinakamilika na vijana wanaendelezwa.

Wadhamini wakuu wa mbio za Kilimanjaro Marathon ni Kilimanjaro Premium Lager wakati Tigo inadhamini mbio za kilomita 21 huku zile za watoto, wazee za kilomita tano zinadhaminiwa na Grand Malt.

Wadhamini wa meza za maji ni Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC, Simba Cement na Maji ya Kilimanjaro wakati wasambazaji rasmi ni GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles na Surveyed Plots Company Ltd (SPC) na Bodi ya Utalii (TTB).

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MARTINEZ ANUKIA CITY**

KLABU ya Manchester City imepata nguvu katika mbio zao za kumshawishi mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 24 baada ya mabingwa hao wa Italia kuripotiwa kumtaka mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram (24), kuziba nafasi yake. ***(Sun)***

**ABRAMOVICH APOKEA OFA**

ROMAN Abramovich tayari amepokea ofa kadhaa zinazokaribia dau la pauni bilioni tatu za kuinunua Chelsea. ***(PA, via Independent)***

**NEVES KUTUA BARCA**

BARCELONA inatarajiwa kumsajili kiungo wa Wolves, Ruben Neves katika kipindi cha majira ya joto, huku mazungumzo kati ya wawakilishi wake yakielezwa kufanyika. Manchester United na Arsenal pia zimeonyesha nia ya kumtaka Mreno huyo mwenye miaka 24 wanaomuhusudu kwa muda mrefu. ***(Mail)***

**KASSIE ATAKIWA EVERTON**

KLABU ya Aston Villa inawataka kiungo wa AC Milan, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 25 na mshambuliaji wa Atletico Madrid, Luis Suarez (35), katika dirisha lijalo la usajili la majira ya joto. ***(Express)***

**BARCA, KASSIE KUTETA**

MAZUNGUMZO ya Barcelona ya kumsajili Franck Kessie yako mbali, huku kiungo huyo wa Milan akiwa kwenye orodha ya wanaowaniwa na Barca wakiwemo walinzi wa Chelsea, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 25 na Cesar Azpilicueta mweye umri wa miaka 32. ***(ESPN)***

**CHRISTENSEN SAFI BARCA**

CHELSEA imempa ofa ya mwisho kujaribu kumbakisha Andreas Christensen pale Stamford Bridge, huku mlinzi huyo wa kimataifa wa Denmark akitajwa kukaribia kusaini mkataba wa awali kujiunga na Barcelona kwenye dirisha lijalo la usajili. ***(90min)***

**WIJNALDUM KUTUA VILLA**

KLABU ya Aston Villa italazimika kulipa pauni milioni 21 kwa ajili ya kiungo wa Paris St-Germain, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 31. ***(Jeunes Footeux, via BirminghamLive)***

**AARONSON ANUKIA LEEDS**

LEEDS United ina matumaini kwamba, uzoefu wa kocha wake mpya, Jesse Marsch akiwa bosi wa Red Bull Salzburg utawasaidia kumnasa kiungo Mmarekani, Brenden Aaronson mwenye umri wa miaka 21 kutoka klabu hiyo ya Austria katika dirisha lijalo la usajili. ***(Star)***

**BELLINGHAM KUBAKI**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18 ameamua kubakia Borussia Dortmund angalau kwa msimu mwingine mmoja. ***(Bild, via Mirror)***

**BOTMAN AKARIBIA MILAN**

AC Milan imeripotiwa imefikia makubaliano na mlinzi wa Lille, Sven Botman, 22, baada ya kukataa kujiunga na Newcastle United. ***(Gazzetta dello***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANTE: WACHEZAJI CHELSEA HATUKUJIANDAA TIMU KUUZWA

### ●●● Nyota hao wasema kwao ni jambo ambalo hawakulitarajia lakini waahidi...

**LONDON,** England

N'GOLO Kante amekiri wachezaji wa Chelsea "hawakujiandaa" kwa habari kwamba, Roman Abramovich anataka kuiuza klabu hiyo.

**Abramovich alitangaza Jumatano kuwa amechukua uamuzi "mgumu sana" wa kuweka klabu hiyo sokoni na kutoa mapato yote kwa waathirika wa vita nchini Ukraine.**

Katika taarifa yake, alisema mauzo hayo "hayatafuatiliwa haraka bali yatafuata utaratibu unaostahili", na kuongeza hataomba mkopo kulipwa na klabu.

Uamuzi wa Abramovich ulikuja huku kukiwa na tishio la vikwazo dhidi ya wafanyabiashara zaidi wa Urusi na watu wenye hadhi ya juu baada ya uvamizi wa Ukraine wiki moja iliyopita.

Bilionea huyo mwenye umri wa miaka 55 alipigwa picha akiwa na rais wa Urusi, Vladimir Putin, siku za nyuma.

Na ingawa ilidaiwa wiki iliyopita Abramovich hajihusishi na siasa, msemaji wa mmiliki huyo wa Blues alisema Jumatatu "anajaribu kusaidia" kufikia suluhu la amani kwa mzozo huo.

Na sasa Kante anakiri wachezaji walishtuka kusikia habari hizo saa chache kabla ya ushindi wao wa Kombe la FA dhidi ya Luton.

Alisema: "Hatukuwa tayari. Ilikuja haraka. Lakini hatuna cha kufanya kwa sababu hatudhibiti vitu hivi.

"Hiyo ina maana kucheza soka kwa ubora wetu kwa ajili yetu, kwa klabu, kwa ajili ya mashabiki. Ni jambo pekee tunalodhibiti na tunataka kufanya hivyo."

Kante, ambaye anatimiza umri wa miaka 31 mwezi huu, amejitolea kikamilifu kuitumikia Chelsea na bado hafikirii kuondoka Stamford Bridge.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 985

MECHI KALI

MBEYA KWANZA FC

VERSUS

MBEYA CITY

1 | 3.05

X | 2.75

2 | 2.75

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:

18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MKHITARYAN ATANGAZA RASMI KUTUNDIKA DARUGA

**ROME,** Italia

NYOTA Henrikh Mkhitaryan yuko wazi kujitolea kwa mradi wa Jose Mourinho wa kuijenga AS Roma baada ya kustaafu kucheza soka la kimataifa.

Baada ya kuichezea mechi 95 timu ya taifa ya Armenia, ambayo haijawahi kufuzu kwa Kombe la Dunia au michuano ya Ulaya, kiungo huyo wa zamani wa Manchester United na Arsenal atamaliza maisha yake ya soka kwenye ngazi ya klabu.

Mkhitaryan alikuwa nahodha wa nchi yake na mfungaji bora wa timu ya taifa baada ya kutikisa nyavu mara 32.

Alitangaza kustaafu kuichezea timu hiyo kwenye mitandao ya kijamii, akiandika ujumbe alioupa jina, "Kwaheri timu yangu ya taifa pendwa." Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliandika: "Nilitaka kushinda kila hatua ya maisha yangu, haijalishi ingekuwa ngumu kiasi gani. Ilikuwa heshima kuchezea taifa langu kwa miaka 15 iliyopita na hata zaidi ya heshima kwa nahodha, kwa miaka sita iliyopita.

"Baada ya mechi 95 za kimataifa na bidii, nimechukua uamuzi wa kustaafu soka langu la kimataifa na timu yangu ya taifa ya Armenia.

Mkhitaryan anakaribia mwisho wa nyongeza ya mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Roma na amefanya vyema kwa kocha mkuu Mourinho.



# Madrid, United zamwania Osimhen

**MANCHESTER,** England

MBIO za kumnasa mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen zinazidi kupamba moto huku Real Madrid wakijiunga na Manchester United kutafuta saini yake, kwa mujibu wa Calciomercato.

Osimhen amefunga mabao 11 katika mashindano yote, na hivyo kufanya baadhi ya klabu kubwa kumwania.

Mshambuliaji huyo wa Napoli anatajwa kuwa na thamani ya takriban euro milioni 80.

Amekuwa na kiwango c kuvutia akicheza hapo Nap na sasa klabu kubwa zinakim zana kuwania saini yake.

Mkataba wa Osimhen pale N poli unamalizika mwaka 20 lakini Madrid na Manchest United ziko tayari kutunisha m suli ili kumnunua katika diris la uhamisho la majira ya joto.

Fowadi huyo mwenye um wa miaka 23 alisajiliwa Nap kwa euro milioni saba akitok Lille mwaka 2020.

,669,400

# AZAM FC KATIKA MTIHANI MWINGINE LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

BAADA ya wiki iliyopita kulazimishwa sare, Azam FC inatarajia kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

**Timu zote zinashuka dimbani zikiwa zimepoteza pointi tano, Azam FC ilipoteza dhidi ya Biashara United halafu ikatoka sare nyumbani dhidi ya Coastal Union kutoka jijini Tanga.**

Azam FC wanashuka dimbani kwenda kutafuta pointi tatu ili kupunguza presha za kuwania nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, John Yona alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo ingawa wanafahamu wataingia uwanjani kucheza dhidi ya timu ngumu.

"Polisi Tanzania ni timu nzuri na tunaingia uwanjani kwa kusaka alama tatu muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea kupambana kubaki katika nafasi ya tatu," alisema Yona.

Naye Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo, alisema baada ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya KMC FC walifanyia kazi mapungufu yao na sasa wamejiimarisha kwa ajili ya kuikabili Azam FC.

"Hatuna majeruhi, wachezaji wote wako fiti na tayari kukabiliana na Azam FC, tunaenda kwa kuwaheshimu wapinzani wetu, tutapambana kutafuta pointi muhimu katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Mketo.

Nahodha wa Polisi, Juma Ramadhani alisema bado wanatafakari jinsi gani ya kwenda kupambana ili kupata ushindi na kuiweka timu yao katika sehemu salama kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Ligi ni ngumu na kila mechi kwetu ni fainali, tunaenda kupambana kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo dhidi ya wenyeji wetu Azam FC," alisema nahodha huyo.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Botswana itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar. **PICHA: TFF**



# Wolper balozi mpya EMINA

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII maarufu wa Bongo Movie nchini, Jaquiline Wolper, ameteuliwa kuwa balozi wa bidhaa za EMINA zinazozalishwa na Kampuni ya Bingwa Laboratory ya jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kutambulishwa kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Wolper alisema hiyo ni fursa kwake huku akiishukuru kampuni hiyo.

Wolper atapeperusha bendera ya EMINA katika kampeni ya USAFI NI AFYA awamu ya pili ambayo itazilenga shule za msingi, sekondari na baadhi ya vyuo vilivyoko katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo elimu na bidhaa za usafi zitatolewa bure.

Msanii huyo aliahidi kuwa balozi mwema wa kampuni hiyo na kuwataka wasanii wanapopewa kazi kama hizo za kuwa mabalozi wa bidhaa kufanya kazi kwa uaminifu na kwa uadilifu ili waendelee kuaminiwa kwenye kazi hizo.

Aliahidi kuwa balozi mwema wa kampuni hiyo na kushiriki katika kampeni ya usafi Mkoa wa Dar es Salaam ambapo watagawa vifaa mbalimbali vya usafi kwa vyuo vikuu, shule za msingi na sekondari

"Ndugu zangu nimewaita hapa kuujulisha umma wa Watanzania na mashabiki zangu kwamba kuanzia leo mimi ni balozi wa bidhaa za EMINA na nitapeperusha bendera ya bidhaa hizi katika kampeni ya usafi ni afya," alisema Wolper.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Bingwa, Emmanuel Mwambete, alisema awamu ya kwanza ya kampeni hiyo ya usafi ni afya ilizinduliwa na Meya wa jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto mwaka jana Kivukoni.


# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/03/22 | 18:00 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.09 | 3.34 |
| 02. 05/03/22 | 18:00 | Newcastle vs Brighton | 2.70 | 3.14 | 2.70 |
| 03. 05/03/22 | 18:00 | Aston Villa vs Southampton | 2.30 | 3.36 | 3.06 |
| 04. 05/03/22 | 18:00 | Norwich City vs Brentford | 2.95 | 3.10 | 2.50 |
| 05. 05/03/22 | 20:00 | Roma vs Atalanta | 2.41 | 3.40 | 2.85 |
| 06. 06/03/22 | 14:30 | Genoa vs Empoli | 2.61 | 3.26 | 2.71 |
| 07. 06/03/22 | 16:00 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 3.31 | 3.06 | 2.32 |
| 08. 06/03/22 | 17:00 | Reims vs Strasbourg | 3.48 | 2.78 | 2.39 |
| 09. 06/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Troyes | 2.29 | 3.48 | 2.93 |
| 10. 06/03/22 | 17:00 | Bologna vs Torino | 2.60 | 3.29 | 2.69 |
| 11. 06/03/22 | 19:00 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 12. 06/03/22 | 19:00 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 2.38 | 3.21 | 2.91 |
| 13. 06/03/22 | 19:30 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.70 | 3.40 | 2.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 05/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4086 | Leicester vs Leeds | 1.77 | 4.10 | 4.00 |
| 16:00 | 5126 | Mbeya Kwanza FC vs Mbeya City | 3.05 | 2.75 | 2.75 |
| 16:00 | 5615 | Osasuna vs Villarreal | 3.55 | 3.35 | 2.08 |
| 17:00 | 5891 | Udinese vs Sampdoria | 1.89 | 3.56 | 4.01 |
| 17:30 | 2158 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.12 | 3.29 | 3.44 |
| 17:30 | 3780 | VfL Bochum vs Greuther Furth | 1.77 | 3.63 | 4.47 |
| 17:30 | 3951 | Hertha BSC vs Eintracht Frankfurt | 3.18 | 3.48 | 2.16 |
| 17:30 | 5393 | Bayern Munchen vs Bayer Leverkusen | 1.39 | 5.57 | 5.97 |
| 17:30 | 5778 | RB Leipzig vs SC Freiburg | 1.55 | 4.27 | 5.37 |
| 18:00 | 1066 | Newcastle vs Brighton | 2.71 | 3.11 | 2.71 |
| 18:00 | 1552 | Norwich City vs Brentford | 2.90 | 3.10 | 2.55 |
| 18:00 | 1885 | Motherwell vs Dundee FC | 2.05 | 3.24 | 3.58 |
| 18:00 | 2403 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.30 | 3.06 | 3.36 |
| 18:00 | 2764 | Preston vs Bournemouth | 3.32 | 3.23 | 2.13 |
| 18:00 | 3076 | Swansea vs Coventry | 2.55 | 3.23 | 2.65 |
| 18:00 | 3524 | Bristol City vs Birmingham | 2.25 | 3.30 | 3.00 |
| 18:00 | 3823 | Middlesbrough vs Luton Town | 1.91 | 3.30 | 3.94 |
| 18:00 | 4022 | Derby vs Barnsley | 2.11 | 3.14 | 3.48 |
| 18:00 | 4095 | Aston Villa vs Southampton | 2.32 | 3.39 | 2.99 |
| 18:00 | 4648 | Ross County vs St Mirren | 2.40 | 3.16 | 2.92 |
| 18:00 | 4663 | Stoke City vs Blackpool | 1.90 | 3.34 | 3.93 |
| 18:00 | 4974 | Reading vs Millwall | 2.89 | 3.23 | 2.35 |
| 18:00 | 5081 | Rangers vs Aberdeen | 1.29 | 5.14 | 9.29 |
| 18:00 | 5200 | QPR vs Cardiff | 2.12 | 3.20 | 3.39 |
| 18:00 | 5468 | Hibernian vs St Johnstone | 1.80 | 3.25 | 4.72 |
| 18:00 | 5881 | Burnley vs Chelsea | 6.81 | 4.20 | 1.48 |
| 18:15 | 5483 | Espanyol vs Getafe | 2.21 | 3.04 | 3.59 |
| 19:00 | 2784 | RB Salzburg vs SCR Altach | 1.11 | 7.49 | 14.41 |
| 19:00 | 3346 | Konyaspor vs Galatasaray | 2.44 | 3.30 | 2.76 |
| 19:00 | 5341 | Lens vs Brest | 1.70 | 3.89 | 4.59 |
| 19:00 | 5742 | Azam vs Polisi Tanzania | 1.80 | 3.08 | 4.53 |
| 19:05 | 3034 | HNK Rijeka vs Slaven Belupo | 1.53 | 4.04 | 5.01 |
| 20:00 | 2191 | BSC Young Boys vs FC Luzern | 1.37 | 5.12 | 6.70 |
| 20:00 | 5157 | Roma vs Atalanta | 2.56 | 3.41 | 2.66 |
| 20:30 | 1653 | Liverpool vs West Ham | 1.30 | 5.61 | 8.81 |
| 20:30 | 1788 | Valencia vs Granada | 1.79 | 3.65 | 4.40 |
| 20:30 | 1975 | Stuttgart vs Monchengladbach | 2.97 | 3.47 | 2.27 |
| 20:30 | 5835 | Kortrijk vs Union Saint Gilloise | 4.83 | 3.84 | 1.65 |
| 20:45 | 5527 | GO Ahead Eagles vs Utrecht | 3.73 | 3.53 | 1.89 |
| 21:00 | 3514 | Portimonense vs Benfica | 6.11 | 4.43 | 1.46 |
| 21:30 | 2989 | New England vs FC Dallas | 1.54 | 4.28 | 5.58 |
| 22:00 | 3523 | Toronto FC vs NY Red Bulls | 2.49 | 3.39 | 2.74 |
| 22:30 | 2006 | Lausanne-Sport vs FC Zurich | 3.89 | 3.75 | 1.81 |
| 22:45 | 3953 | RFC Seraing vs Brugge | 6.30 | 4.63 | 1.43 |
| 22:45 | 5794 | Cagliari vs Lazio | 3.44 | 3.39 | 2.11 |
| 23:00 | 3469 | Real Madrid vs Real Sociedad | 1.68 | 3.81 | 4.95 |
| 23:00 | 4197 | Nice vs Paris St Germain | 3.78 | 3.68 | 1.89 |
| 23:00 | 5473 | Feyenoord vs Groningen | 1.26 | 5.50 | 9.81 |
| 23:30 | 2561 | Sporting Lisbon vs FC Arouca | 1.25 | 5.54 | 10.88 |
| 23:30 | 5748 | Sporting Kansas City vs Houston Dynamo | 1.92 | 3.61 | 3.81 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Machi 5, 2022

Nipashe




## Madrid, United zamwania Osimhen

UKURASA 22



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele mara baada ya kutua kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwanza tayari kuwakabili Geita Gold FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho jijini humo. **PICHA: MTANDAO**

## Waamuzi Ligi Kuu waahidi makubwa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwapo na malalamiko ya mara kwa mara, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi Nchini, Nassor Hamdoun, amesema raundi ya 16 ya Ligi Kuu Tanzania Bara haikuwa na 'kelele' kuhusiana na waamuzi kutokana na maofisa hao kujitathmini.

Hamdoun, mwamuzi wa zamani wa kimataifa, aliliambia gazeti hili kuwa semina ya siku tatu iliyoendeshwa hivi karibuni baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza imeleta matunda chanya na kuahidi hali hiyo itaendelea hadi mwisho wa msimu.

Mwenyekiti huyo alisema kwa sasa waamuzi wameongeza umakini kwa sababu wanafahamu wanahitaji kupata bingwa wa ligi ambaye amepata ushindi wa halali na hiyo itapunguza malalamiko.

"Ni kweli tumemaliza raundi ya 16 na kuendelea bila malalamiko, tunashukuru na lazima tupongezane. Ni kwa sababu tumejitathmini, katikati ya ligi waamuzi huwa tuna semina kwa ajili ya kuangalia changamoto zilizojitokeza katika mzunguko wa kwanza ili zirekebishwe, na yale mazuri tuyashikilie," Hamdoun alisema.

Kuhusu mechi zinazofuata, kiongozi huyo alisema kuwa matumaini yake ni kuendelea na kuifanya Ligi Kuu Tanzania Bara iendelee kuwa bora kama ilivyo hivi sasa ambapo ni moja kati ya ligi 10 bora barani Afrika.

"Tunataka kuwafanya waamuzi wetu wawe wanachezesha kwa wingi nje ya nchi, na hatutasita kutoa adhabu pale tunapoona wanakwenda kinyume na inavyotakiwa.

Kuhusiana na malipo, Hamdoun, alisema waamuzi wa Tanzania ni moja kati ya wanaolipwa vizuri hapa barani Afrika, na sasa wanalipwa kwa wakati na kama hali ya ucheleweshaji itatokea, basi hutokana na sababu zisizozuilika.

# Mayele : Ni msimu wa Yanga

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

## ●●● Mshambuliaji huyo asema pia amejipanga kuchukua tuzo ya ufungaji bora na...

WAKATI kikosi cha Yanga kikitua salama jijini Mwanza, mshambuliaji wa kimataifa wa timu hiyo, Fiston Mayele ameweka wazi anapambana kuhakikisha anaibuka na tuzo ya ufungaji bora lakini pia akilenga kuisaidia klabu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Yanga imetua Mwanza kwa ajili ya mechi yake dhidi ya wenyeji Geita Gold FC kutoka mkoani Geita kuchagua Uwanja wa CCM Kirumba kutumika hapo kesho.**

Mayele ameshafunga mabao tisa akiwa nyuma ya mshambuliaji wa Namungo FC, Reliants Lusajo ambaye ametikisa nyavu za wapinzani mara 10.

Mayele aliliambia gazeti hili jana kuwa malengo yake makubwa ni kuona Yanga inapata matokeo mazuri katika kila mechi huku akiongeza umakini wa kutumia nafasi za kufunga mabao anazopata.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, nitapambana kutimiza malengo yangu kuhakikisha natumia vizuri nafasi tunazopata kuendelea kufunga mabao na timu yangu kufikia malengo yetu," alisema Mayele.

Mkongomani huyo alisema wakati akihitaji kuchukua tuzo ya ufungaji bora angependa kuona wanachama na mashabiki wa timu hiyo wanaendelea kufurahi.

"Kila mechi ni ngumu na kila timu imejipanga kutafuta matokeo mazuri hasa kipindi hiki cha mechi za duru la pili, kwetu tunahitaji kuendelea kutafuta pointi muhimu ili kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa ligi," alisema Mayele.

Aliongeza hana presha na kiwango chake cha kufumania nyavu na anachongalia zaidi ni kupambana katika kila mechi ili wapate kile wanachokitarajia.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana kabla kikosi hicho hakijaondoka, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedrick Kaze alisema kwanza kupambana kupata pointi tatu muhimu.

"Tunakwenda kukutana na timu ya Geita Gold, lengo leti katika mechi hiyo ni kupata matokeo mazuri na kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wako katika hali nzuri na kila mmoja anahitaji kuona wanaendeleza kasi ya ushindi waliyonayo msimu huu.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu msimu huu kila timu imejipanga vizuri na inahitaji kujipusha na janga la kushuka daraja.

"Hali za wachezaji ambao walikuwa majeruhi zinaendelea vizuri, baadhi yao wanakaribia kurejea kikosini na kilichobaki ni kusubiri taarifa kutoka kwa daktari wa timu ili kufahamu tutakaowakosa," Kaze alisema.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kikosi kimeondoka jijini kikiwa na ari kubwa na kuongeza lengo lao ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na Kombe la FA.

"Timu yetu imejipanga vizuri kuelekea katika mchezo huo, tunaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi siku ya mchezo, tuko tayari kwa mapambano," alisema Bumbuli.

Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Azam FC kuwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Azam Complex huku kesho Ruvu Shooting ikiwaalika Biashara United, Coastal Union ikiwafata KMC na Simba ikiwaalika Dodoma Jiji FC keshokutwa.

9 770856 541002 >